


Butiku aonya yanayotokea Kenya, Gen Z

- Ashauri Katiba ifuatwe,
- wananchi waheshimiwe

Soma Uk. 4

Donald Trump akiwa ameking-wa na maofisa usalama baada ya risasi kuparaza sikio lake katika mkutano wa hadhara huko Pennsylvania katika jaribio la kumuua. (Picha kutoka Getty Images)

Risasi yampaisha Trump



Soma Uk. 33

Kila mchezaji Hispania kupata bilioni 1/-



Soma Uk. 39

Ndani

Safu kamambe

- Askofu Bagonza
- Dkt. Kijo Bisimba
- Evarist Chahali
- Jicho la Tai

Pambazuko laibua serikali kujitetea ufisadi mnadani

VIONGOZI wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wamefanya ziara kwenye Mnada wa Kimataifa wa Mifugo Pugu, Dar es es Salaam, kufanya ukaguzi na uhakiki...

Soma zaidi Uk. 8

African journalism. 13 JULY 2024 | ISSUE 187

The Continent

Mtuhumiwa uhalifu wa kivita anaponda raha mafichoni

Uk. 31



Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Uk. 12

Tahariri/Katuni

Ni jukumu la wote kutokomeza Ukimwi

TANZANIA ni miongoni mwa nchi tano za Afrika ambazo zinatajwa kuwa zitakuwa zimetokomeza maambukizi mapya ugonjwa wa Ukimwi ifikapo mwaka 2030.

Inaelezwa na Umoja wa Mataifa (UN) kuwa Bara la Afrika, hasa eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara ndiko asilimia 65 ya watu wote wenye maambukizi ya Ukimwi duniani wanaishi, hivyo bado kuna kazi kubwa ya kufanya kupuguza ida-di hii.

Tanzania inatajwa kufikia lengo ushindi wa mapambano dhidi ya Ukimwi kwa uwiano wa '95-95-95.'

Kwamba Umoja wa Mataifa kupitia shirika lake la kupambana na Ukimwi (Unaids), unabainisha kwamba katika Tanzania, asilimia 95 ya watu wanaoishi na ugonjwa huo wanajua hali zao, asilimia 95 ya watu wanaojua hali zao wanatumia dawa kurefusha maisha, na asilimia nyingine 95 ya watu wanaopata matibabu wamevifubaza virusi vinavyoambukiza ugonjwa huo uliotikisha dunia kwa miongo mingi.

Hata hivyo, hatua hiyo ya kutokomeza ugonjwa huo haitakuwa na maana ikiwa kila nchi, ikiwamo Tanzania itabweteka na kukaa kusubiri serikali ndiyo ifanye kila kitu kutokomeza ugonjwa huo.

Ni vyema kila mmoja wetu kuwa mwangali-fu ili kuhakikisha Tanzania kweli inaungana na nchi zingine kutokomeza maambukizi mapya ifikakpo 2030.

Ikiwa kila Mtanzania atajikita kulinda afya yake na ile ya wengine, uhakika ni kwamba Ukimwi hautakuwa janga tena kutisha hatma ya uhai wa taifa letu.

Pambazuko tunaendelea kuhimiza watu kupima kujua afya zao na kujiepusha na ngono, ikiwa kuna ulazima wa kufanya ngono, basi wahusika wahakikishe wanazingatia matumizi sahihi ya kinga.

Tunaamini kuwa mwisho wa kusambaa kwa ugonjwa wa Ukimwi ni fursa ya urithi wenye nguvu ya kipekee kwa ustawi wa Tanzania na watu wake.

Inawezekana, kila mtu atende wajibu wake.



Maadhimisho



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisikiliza wimbo wa kuabudu wakati alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Maadhimisho ya Miaka 85 ya Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) kwenye uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Jisajili kupata Pambazuko bure


- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz



Butiku aonya yanayotokea Kenya, Gen Z



Joseph Butiku, akizungumza na wahariri wa Pambazuko wakati wa mahojiano maalum na gazeti hili ofisini kwake jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Fidelis FELIX)

Na Waandishi WETU

VUGUVUGU la vijana kutaka mabadiliko kumetikisa Kenya, huku kiongozi wake, Rais William Ruto akiamua “kuweka maguvu ya dola chini” ili kutekeleza matakwa ya wananchi.

Hali hiyo ya vuguvugu iliyosababisha vifo vya waandamanaji, imemtisha Joseph Butiku, aliyekuwa msaidizi wa karibu zaidi wa Rais wa Kwanza wa Tanzania - Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Butiku ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, ameonya kuwa mambo yanayoendelea kutokea Kenya hivi sasa, yanaweza pia kuikumba Tanzania iwapo Katiba haitafuatwa na kuheshimiwa.

Ili kuepuka hali hiyo, amewashauri viongozi kuheshimu Katiba na misingi yake ikiwa ni pamoja na kutenda haki kwa wananchi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Butiku ameyasema hayo Ijumaa iliyopita,

alipokuwa akizungumza na Pambazuko katika mahojiano maalum yaliyofanyika ofisini kwake, Dar es Salaam.

Msiri huyo wa Baba wa Taifa amesema anaamini vuguvugu hizo na hata vurumai, zimetokana na kutofuata Katiba na serikali kudhani iko juu ya wananchi.

“(Kenya) hawafuati Katiba. Hata hapa kwetu tusipofuata Katiba yatatokea yanayotokea Kenya. Hata katika kuripoti kwenu (waandishi), mnatakiwa kufuata Katiba, mripoti watu wafuate haki, watu waheshimu Katiba, mripoti watu waache rushwa,” amesema Mzee Butiku akitoa maoni yake kuhusu vuguvugu linaloendelea Kenya.

Hivi Karibuni, mamilioni ya raia wa Kenya, waliandamana katika miji mbalimbali nchini humo wakipinga mwenendo wa serikali yao kwa kile walichosema imewasababishia magumu wa maisha.

Inaendelea Uk. 7

Rais Samia asiwe mkweli saanaaaa!

Na Igo Al

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ametakiwa kupunguza kiwango cha ukweli kila anapozungumza na wananchi.

Ushauri huo umetolewa usiku wa kuamkia leo na mtumishi wa shirika la umma mstaafu, Mzee Tai wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mustakabali wa Tanzania na watu wake.

Mzee Tai ambaye mara zote anapozungumza masuala ya kitaifa, mbele ya waandishi wa habari hupendelea kuvaa tisheti yake ya kijani – yenye picha ya Rais Samia na maandishi yanayosomeka; Mitano tena kwa Mama, aliomba kufikishiwa ujumbe wake kwa kiongozi wa Tanzania, akimsihi kupunguza kusema ukweli.

Kwamba Rais Samia anapokuwa mkweli sana, baadhi ya watu anaowaogoa wanashindwa kumwelewa na kufanya “ndivyo sivyo” – hivyo kumvurugia.

Mzee Tai amesema ukweli uliopitiliza wa kiongozi huyo wa Tanzania, mara nyingi umekuwa ukimponza na kuonekana “anaruhusu-ruhusu tu mambo.”

“Hebu fikirieni nyie waandishi wa habari, Rais Samia alisema kuwa “kila mtu atakula kwa urefu wa kamba yake, kauli hii ni kama imeruhusu watu kuendelea kula rushwa, sasa haya ndiyo nasema, mweyekiti wetu wa chama anachukuliwa sivyo-ndiyo,” amesema.

Mbali na hilo la urefu wa kamba, Mzee Tai anasema kuwa lipo jingine ambalo Rais Samia alimweleza mkuu wa Tiaraei, kwamba anawatambua wezi wote wa huko, kwa kuwa labda naye alikuwa miongoni mwao.

“Mimi najua, nimekuwa huko serikalini kwa muda mrefu, na hata mnaniona

hapa nimefikia kustaafu, mjue natambua mengi, ndiyo maana hata hilo la Mama (Rais Samia) kumzungumia bosi wa Tiaraei, huenda kuna ka ukweli, lakini kwanini asema? Amehoji Mzee Tai.

Mzee Tai amesema ujumbe huo wa Rais Samia kwa bosi wa Tiaraei, usigeuke na kuchukuliwa kuwa ni kweli, kwani Watanzania watajumlisha moja na moja na kuja na jibu kwamba “kumbe huyo mpya, naye ni walewale.”

Mgeni atua Pambazuko...mnamfahamu?



Ni asubuhi ya wiki iliyopita, ndege huyu alibisha hodi ofisi za gazeti la Pambazuko. Alikutwa jirani na mlango na hakuwa na woga wala wasiwasi wa kukutana na watu. Alikaa kwa muda wa dakika kama saba na kuruka. Kila mmoja alishangaa kuona aina hiyo ya ndege, na hakuna aliyetambua kuwahi kumuona. Sasa inaulizwa, je, huyu ni aina gani ya ndege? Anapatikana wapi zaidi? Msaada tafadhali kutoka kwa wasomaji wetu. Tutumie majibu kupitia namba hii: 0744 768 263 (Picha na Mpigapicha Wetu).

Tangazo

JIMBO KATOLIKI KIGOMA

SHULE YA SEKONDARI YA
MT.BAKANJA, MUHINDA

SLP 186, BUHIGWE – KIGOMA



Nafasi za Masomo mwaka 2025

- Kidato cha Kwanza
- Wanaohamia vidato vyote
- Shule inapokea wanafunzi wa dini zote
- Shule inafanya mitihani ya Sayansi kwa Vitendo
- Shule ni ya Bweni na Mchanganyiko (ME na KE)
- **Ada zetu ni nafuu na hulipwa kwa awamu NNE.**



Mtihani wa kujiunga: Tarehe 17/09/2024 na 21/09/2024 katika vituo vilivyooneshwa kwenye fomu ya kujiunga.

Mafunzo ya Awali (pre form I) yataanza tarehe 01/10/2024 – 18/12/2024, kwa gharama ya Tsh. 150,000/=

Fomu za kujiunga zinapatikana Katika Parokia zote za Jimbo la Kigoma, na online kupitia namba za mawasiliano:

0612 168 058 / 0760 3464 44
0760 464 344 / 0620 287 431

Ufanisi katika Taaluma, Michezo na kazi za Mikono

Butiku aonya yanayotokea Kenya, Gen Z

Inatoka Uk. 4

Wakati wa vuguvugu hilo, linaloendeshwa zaidi na vijana kwa njia ya maandamano, awali walishinikiza kufutwa kwa Sheria ya Fedha iliyokuwa imepitishwa na Bunge wakiilalamikia kuwa inaongeza kodi na kusababisha maisha kuwa magumu.

Kutokana na maandamano hayo, Rais Ruto, aliamua kurudisha bungeni muswada wa sheria hiyo baada ya kupitishwa, na siku chache baadaye akavunja Baraza la Mawaziri kama sehemu ya utekelezaji wa madai ya waandamanaji hao vijana waliopachikwa jina maarufu sasa la Gen Z.

Wakati wa maandamano hayo, watu zaidi ya 40 wameripotiwa kuuawa na wengine wakijeruhiwa huku mali za umma na watu binafsi zikiharibiwa.

Mbali na hofu yake kwa yanayotokea Kenya, Butiku alizungumzia uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani – wa Tanzania, unaotarajiwa kufanyika mwakani huku akisema wapigakura wanatakiwa kuwa makini ili kuchagua viongozi wenye sifa za kuongoza.

Amesema, bila kuwa na umakini, viongozi wengi watachaguliwa kwa rushwa, hatua ambayo haina mustakabali mwema kwa Tanzania.

“Katika suala la uchaguzi, ni nafasi ya kupata viongozi bora watakaofuata Katiba. Hiyo ndiyo nafasi ya kusema huyu anafaa na huyu hafai...”

“Ni nafasi ya kuitumia vizuri, usihongwe kuchagua kiongozi aliyetoa rushwa,” ameingiza.

Kuhusu maandamano ambayo yamekuwa yakifanywa na baadhi ya vyama vya siasa – hasa Chadema, Butiku ameonyesha kutoridhishwa nayo akisema hayatoi suluhisho la matatizo mengi yanayowakabili Watanzania hivi sasa.

Kutokana na hali hiyo, ameshauri viongozi wa kisiasa waanze utaratibu wa kuzungumzia matatizo ya wananchi na kutafuta njia mbadala za kuyatatua badala ya kuwahamasisha washiriki maandamano mitaani.

“Vyama vya siasa ni vyama vya kusaidia kuboresha mambo mbalimbali na kamwe hawezi kuwa vyama vya maandamano kila waka-

ti kwa sababu maandamano ni staili ya wanayonge...”

“Kama kuna mahali panakosewa, hebu tuzungumze ili twende mbele kwa sababu watu wetu ni masikini mno wanahitaji kusaidiwa...”

“Nasema hivyo kwa sababu tangu tuanze huu mfumo wa vyama vingi, haujafanya kama tunavyotaka, yaani huko bungeni watu wanapigana na mfumo wenyewe haujaleta maji na haujaleta mambo mengi mazuri...”

“Vyama vingi siyo ugomvi, bali ni kuzungumza kama wanavyofanya watu wazima. Msipokubaliana kwenye baadhi ya mambo ambayo wengi wameshinda, basi mnasonga mbele,” akasisitiza Butiku.

Wakati huohuo, Butiku alizungumzia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na kusema anaridhishwa nao kwa kuwa kuna mambo mengi ameyabadilisha.

“Mama (Samia) anakwenda vizuri kwa sababu lazima muelewe kwamba amerithi nchi kutoka kwenye msiba na kabla ya hapo mnajua alikuwa makamu wa rais...”

“Mnajua hata mzee mwenye nyumba aki-fariki, kuna baadhi ya watoto wanaanza kuleta machachari machachari, lakini nasema mama anakwenda vizuri...”

“Mama ameruhusu watu kuzungumza ila msiniulize nalinganishaje utawala huu na uliopita kwa sababu hiyo siyo kazi yangu...”

“Mama amepanua wigo wa mazungumzo na ameshasema Watanzania tuzungumze mambo yote yaliyoko mioyoni mwetu ili aweze kuyajua...”

“Vyama vya siasa amevisikiliza ikiwamo kuruhusu mikutano ya hadhara na maandamano ambayo sasa mnayashuhudia,” amesema Butiku.

(Mahojiano kamili na Mzee Butiku yatachapishwa katika toleo lijalo la Pambazuko)





Habari

Pambazuko laibua serikali kujitetea ufisadi mnadani



Mnada wa Ng'ombe Pugu

Na Mwandishi WETU

VIONGOZI wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wamefanya ziara kwenye Mnada wa Kimataifa wa Mifugo Pugu, Dar es Salaam, kufanya ukaguzi na uhakiki wa vibali vya tozo na mifugo inayoingia na kutoka.

Hatua hiyo inakuja siku chache baada ya gazeti hili, Pambazuko, kufichua ufisadi unaofanywa na baadhi ya watumishi waliopo kwenye mnada huo kwa kuinyima mapato serikali, huku wakin-ufaika binafsi.

Ziara ya viongozi hao wakiongozwa na naibu katibu mkuu wa wizara hiyo, Prof. Daniel Mushi imefanyika Ijumaa - Julai 12, 2024 ikiwa ni siku nne baada ya gazeti hili la Pambazuko kuripoti kuhusu kuwepo kwa vitendo vya ufisadi.

Uchunguzi uliofanywa na Pambazuko ulibaini kuwa miezi saba baada ya waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega kuagizo kuondolewa kwa baadhi ya watendaji wa mnada huo, hakuna kilichotekelezwa kikamilifu.

Katika ziara yake ya Januari 23, mwaka huu, Ulega aliagiza kuondolewa kwa wafanyakazi wote kwenye mnada huo, kusimamia upatikanaji wa maji wa uhakika kwa ajili ya mifugo na binadamu.

Pia aliagiza kuboresha taa kwa ajili ya kuimarisha mwanga kwenye eneo la mnada huo wa kimataifa unaofanya kazi kwa saa 24 na kuhakikisha kunakuwa na barabara ya uhakika kuelekea kwenye mnada huo.

Gazeti hili liliripoti kuwa licha ya maelekezo hayo ya waziri, bado rushwa na ubadirifu ulikuwa ukiendelea kushamiri na kuchepusha mapato ya serikali mifukoni mwa wachache.

Uchunguzi huo uliofanywa na waandishi wa Pambazuko walioweka kambi kwa siku 13 katika eneo la mnada huo na kubaini kupuuzwa kwa maagizo hayo.

Pambazuko lilibaini kuwepo watumishi wachache waliohamishwa, huku vinara wa “upigaji” mnadani hapo kutokuguswa.

Akiwa katika ziara yake ya mwishoni mwa wiki, Prof Mushi alizungumzia tatizo la uhaba wa maji pekee, akisema kuwa ni kweli hakuna maji ya kutosha, hivyo wanaendelea na utaratibu wa kuchimba visima katika eneo hilo ili kuongeza upatikanaji wa maji.

Kuhusu ufisadi mnadani

Akizungumzia taarifa kuhusu ufisadi wa kutisha unaoendelea mnadani hapo ambao husababisha zaidi ya Shilingi milioni 100 kupotea kwa kuingia mifukoni mwa watu kila mwezi, Prof. Mushi alishindwa kujadili na badala yake akasema; “tumezisoma taarifa kwenye gazeti” -bila kujaja ni Pambazuko.

Prof. Mushi alikuwa akizungumza Katika kipindi cha Aridhio kinachorushwa na televisheni ya TBC, na kudai kuwa taarifa hizo “zimewasikitisha sana.”

“Tulifanya mabadiliko ya timu nzima pale mnadani na kwa taarifa tulizonazo ni kwamba ufisadi huo unaozungumzwa haujathibitishwa.”

“Huenda kuna uzembe kwenye usimamizi wa ukusanyaji wa mapato unaosababisha mianya hiyo, lakini kwa kipindi cha miezi sita iliyopita, mapato yameongezeka maradufu, tutaendelea kufuatilia na kuweka mfumo mzuri wa kupata taarifa kutoka ngazi ya chini kabisa,” alisema.

Mezani kwa Chahali



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mombo ana kibarua kigumu cha uchaguzi

ALHAMISI ya wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan alimtea Selemani Abubakar Mombo kuwa mkurugenzi mkuu mpya wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu, ilieleza kuwa aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Balozi Ali Siwa, amestaafu.

Ndugu Mombo anakuwa kurugenzi mkuu wa 13 tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo nyeti nchini Tanzania

Orodha ya wakurugenzi wakuu waliopita ni kama ifuatavyo;

Balozi Ali Siwa (Agosti 2023 – Julai 2024); Said Masoro (Januari 2023 – Agosti 2023); Diwani Athumani (2019 – Januari 2023); Dkt. Modestus Kipilimba (2016 – 2019); Rashid Othman (2005 – 2016); na Cornel Apson Mwang'onda (1995 – 2005).

Wengine ni Luteni Jenerali Imran Kombe (1983 – 1995); Dkt. Augustine Mahiga (1980 – 1983); Dkt. Hassy Kitine (1978 – 1980); Dkt. Lawrence Gama (1975 – 1978) na Emilio Mzena (1961 – 1975)

Mombo anaweza kuweka rekodi ya kipekee kama mtu aliyetabiriwa sana siku za nyuma kuwa huenda angeteuliwa kuwa mkuu wa taasisi hiyo.

Na kwa hakika, mara baada ya Rais Samia kuingia madarakani, Machi mwaka 2021, jina la Mombo lilisikika kwenye mitandaoya kijamii kuwa huenda ndiye angeteuliwa kuwa kiongozi mkuu wa idara hiyo yenye majukumu nyeti na muhimu kwa mustakabali wa Tanzania na watu wake.

Utaratibu usiokuwa rasmi, na hii siyo kwa

Tanzania, tu bali nchi nyingi duniani, ni kwamba rais mpya hutarajiwa kuwa atateua mkuu mpya wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Hii inatokana na ukweli kwamba kiongozi mkuu wa idara hiyo ndiye mshauri mkuu wa rais kuhusu usalama wa taifa husika.

Ingawa maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa hawapaswi kufahamika hadharani - kirahisi, ukweli kwamba Mombo amewahi kushika nyadhifa nyingi “za uraiani” umechangia kufahamika kwake kuwa ni mtumishi wa taasisi hiyo.

Lakini kubwa zaidi ni sifa miongoni mwa watu wanaomfahamu kuwa ni “mtu wa watu”, ambayo inatarajiwa kuwa mtaji wake muhimu katika uongozi alioanza kuutumikia.

Asili ya taaluma ya uofisa usalama wa taifa husababisha maofisa wachache wanaofahamika, kuogopwa kupindukia na hiyo huathiri upatikanaji wa taarifa za kiusalama, hasa kwa sababu chanzo muhimu cha taarifa hizo ni wananchi wenyewe.

Moja ya changamoto kwa Mombo ni uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu Oktoba mwakani.

Hata hivyo, inatarajiwa kuwa uzoefu wake utamwezesha yeye binafsi na taasisi anayoongoza kulivusha taifa la Tanzania salama, kwani ana mtaji mkubwa wa watu.


Haiaminiki kama Mombo anaweza kubadilika na kuwa mbabe na mtawala zaidi baada ya kupata dhama hiyo, kwani haijawahi kuwa tabia yake.

Kila la heri Ndugu Mombo



Rais Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Selemani Abubakar Mombo. (Picha na Ikulu)

https://instagram.com/evarist_chahali



Tafakuri ya Bagonza

Kutendewa wema na usiyemtegemea ni zaidi ya kujali

Na Dkt. Benson BAGONZA

JUMAPILI ya saba baada ya Utatu, tumekusanyika Mtaa Kamushule, Runyaga, Kituntu, Karagwe, Kagera.

Kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ni juma la “kujali wengine.” Tumekuwa na wageni marafiki wanaojali kutoka Ujerumani na Uingereza.

Injili imetukumbusha Msamaria Mwema. Alimkuta majeruhi ametupwa. Akamjali, akampeleka nyumba ya wageni na kumtunza.

Huyu alipitwa na kuhani na Mlawi. Jamii ilitegemea hawa wamjali, lakini hawakufanya. Msamaria, mlalahoi, aliyetengwa kijamii, akamjali. Shtuka.

Somo la mahubiri limetoka 2 Samweli 9:9-11. Kulielewa yakubidi ujue mtiririko. Ni huu:

Kwamba Mfalme Sauli alichemsha! Kichaa cha madaraka kikamzidi na mabega yakazidi kichwa. Wananchi wakamkataa na Mungu akamkataa.

Kwamba Mungu akamteua Daudi, mtoto wa mwisho wa Mzee Yese, akiwaacha kaka zake saba. Daudi mwenye miaka 15, mchungu kondoo, akawa mfalme wa pili wa Israeli. Mungu akamtuma Nabii Samueli amtie Daudi mafuta awe mfalme.

Kwamba Mfalme Sauli akamtafuta Daudi amuue. Akaonywa, hakuonyeka. Hata mtoto wake wa kwanza Jonathan, akamuonya baba yake aachane na mpango wa “kumpoteza” Daudi. Hakusikia.

Kwamba Jonathan akajiunga na Daudi na kuapizana naye kumsaidia ili asiawe na Sauli. Dola ikagawanyika vipande. Mfalme Sauli aliyetumbuliwa, akajiua. Jonathan pia alikufa akiacha watoto yatima mmojawapo aliitwa Mefibosheth. Alikuwa mlemavu wa mguu.

Kwamba Mfalme Daudi akaletewa Mefi-

bosheth mbele yake katika operesheni ya “kuwashughulikia” waliokuwa watu wa Mfalme mbaya Sauli. Ilitegemewa asisaidiwe, lakini;

Kwamba Mfalme Daudi akampokea; akamrudishia mali zake, akampatia watumishi wa kumtumikia, akaagiza daima akae naye meza ni na kula naye. Zaidi, awe sawa na wana wa mfalme! Kwa nini?

Kwamba ni mtoto wa Jonathan; mtoto wa Sauli; aliyemuasi baba yake na kumsaidia aliyepindua baba yake. Daudi akakumbuka wema aliotendewa na Jonathan, naye akamjali mtoto wake ambaye ni mjukuu wa mtesi wake (Sauli). Tuko pamoja?

Tunajifunza nini?

Kwamba wema ni akiba, hata ubaya ni akiba. Kuna siku vitakurudia.

Kwamba Ukristo si kutenda uliyoagizwa tu. Ni kutenda zaidi ya uliyoagizwa (juu ya viwango). Kutoiba ni kutimiza amri. Lakini kutoiba na ukazuia wezi ni zaidi ya agizo.

Kwamba kujali ni zaidi ya huruma. Kuna watu wana huruma lakini inaishia mioyoni mwao. Kujali ni kutenda na yaweza kuhatarisha usalama wako. “Machawa” hawapendi mfalme anayejali.

Siku ilikuwa njema. Tukala mchele na baadaye tukapeana zawadi.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.





Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni taa-sisi kongwe nchini Tanzania, iliyojengwa kwenye misingi imara tangu kuanzishwa kwake Juni 30, 1966 huko Visiwani Zanzibar.

Kwa zaidi ya miaka 50 ya utendaji, PBZ imejikita kutoa huduma bora za kifedha kwa wananchi. Hivi karibuni, PBZ imezindua tawi jipya mkoani Morogoro, hatua inayotarajiwa kuwa kichocheo kikubwa cha kukua uchumi katika eneo hilo.

Morogoro ni moja ya mikoa muhimu katika uzalishaji wa chakula na mazao mbalimbali nchini Tanzania. Mkoa huu unaongoza katika uzalishaji wa mbogamboga na viungo, ambavyo ni muhimu kuimarisha sekta ya kilimo.

Ufunguzi wa Tawi la PBZ Morogoro utasaidia wakulima na wafanyabiashara kupata huduma za kifedha karibu nao, hivyo kurahisisha kupatikanika mikopo na huduma nyingine za benki.

Mwendelezo wa PBZ kufungua matawi katika mikoa mbalimbali kama Dar es Salaam, Dodoma, Mtwara, na baadaye Mbeya, ni ishara ya nia njema ya kudumisha Muungano wa Tanzania.

Hii ni juhudi za viongozi wetu kuimarisha mshikamano wa kitaifa na kushirikiana katika kujenga taifa lenye ustawi na maendeleo kwa wananchi wote.

Hatua hizi zinaakisi dhamira ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma za kijamii bila ubaguzi, na kujenga maisha bora kwa wote.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa PBZ, Arafat Haj, benki hii ni ya saba kati ya benki 47 nchini kwa utoaji bora wa huduma za kifedha.

Hii inaonesha jinsi PBZ ilivyojipanga vyema kuhakikisha inatoa huduma bora na za kisasa kwa wateja wake.

Tawi la PBZ Morogoro litakuwa kiungo muhimu kati ya matawi ya Dar es Salaam na Dodoma, hivyo kusaidia kuimarisha mtandao wa huduma za kifedha katika maeneo haya.

Morogoro ni mkoa wenye fursa nyingi za ki-maendeleo, ikiwemo ukubwa wake na vivutio vya kitalii kama mbuga za Mikumi, Nyerere na Udzungwa.

Aidha, mkoa huu una utitiri wa vyuo vikuu

Morogoro wasilaze damu fursa za PBZ




na vya kati, jambo ambalo linaweza kuchangia kuongeza mahitaji ya huduma za kifedha.

PBZ inaweza kutumia fursa hizi kujitana na kuongeza huduma zake katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Morogoro, hivyo kusaidia wananchi wengi zaidi kunufaika na huduma zake.

Ufunguzi wa tawi la PBZ Morogoro ni hatua muhimu inayotarajiwa kuleta mafanikio makubwa kwa wakazi wa mkoa huo na maeneo jirani.

Kwa kutumia vizuri fursa zilizopo, PBZ inaweza kusaidia kukuza uchumi wa mkoa na kuimarisha ustawi wa wananchi kwa kutoa huduma bora za kifedha.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Ana kwa Ana

Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

FREDERICK Tluway Sumaye ameweka rekodi ya kuwa mwasisia ambaye alidumu katika nafasi ya waziri Mkuu wa Tanzania kwa kipindi kirefu cha miaka kumi.

Sumaye pia ni mwanasisia mkongwe aliye-wahi kuwa Mbunge wa Hanang kwa miaka 22; kuanzia mwaka 1983 hadi 2005.

Mwaka 1985 Rais Ali Hassan Mwinyi, alim-teua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Ushirika, wadhifa aliushika hadi mwaka 1994 alipoteuliwa kuwa waziri kamili wa wizara hiyo hadi 1995.

Mwaka 1992 wakati wa siasa za vyama vingi zilipoanza, Sumaye ni miongoni mwa vigogo wa CCM waliopambana na upinzani mkali kutoka kwa Siringi Mangi Nathael wa NCCR-Mageuzi mwaka 1995, lakini baadaye alishinda tena jimbo hilo, ushindi uliomrudisha bungeni na hapo ndipo Rais Benjamin Wiliam Mkapa, akamteua kuwa Waziri Mkuu nafasi aliyodumu kwa miaka yote kumi ya awamu ya tatu.

Wiki iliyopita, mwandishi wetu **Elizabeth HOMBO** alimhoji mwanasisia huyu ambaye amezungumzia masuala mengi kuhusu Tanzania na wananchi wake, endelea...

Pambazuko:

Ukiwa Waziri Mkuu chini ya Rais Benjamini Mkapa wakati mnaondoka madarakani mlifanikiwa kuiacha nchi ikiwa na uchumi mkubwa imara, lakini hali hiyo hivi sasa haiendani na kasi ya kupungua

kwa umasikini. Unadhani ni kitu gani kimekwenda tofauti?

Sumaye: Siwezi kusema nini kilikwenda tofauti. Kwanza ukitaka hilo lifanyike unaangalia uchumi tulipoukuta ulikuwa na hali mbaya. Kwa hiyo ni lazima kama unataka uchumi ukae vizuri lazima uweke stability (utulivu) katika macro economy (uchumi mkubwa) na ndiyo kazi kubwa tuliyoifanya.

Lakini wakati huohuo hatukuwa pia tumeacha micro economy (uchumi mdogo), tulikuwa tunashughulika nao.

Ili kuweka nguzo kuu ya uchumi ikae sawasawa, ilituchukua muda mrefu kwa sababu hali ya uchumi ilikuwa mbaya sana wakati tunaingia kuongoza.

Na ndiyo maana miaka mitano ya mwanzo hali ilikuwa mbaya sana na kama utakumbuka wananchi walikuwa wameanza kusema kwamba Mkapa ameleta 'ukapa,' lakini actually (kwa kweli) tulikuwa tunarekebisha uchumi na kurekebisha uchumi unaanza na macro economy ili zile nguzo kuu za uchumi ziwe imara.

Sasa ukishaweka zile nguzo imara baadaye unakuja kuweka nyama, hivyo inakuwa rahisi na ikumbukwe kuwa micro tulikuwa hatujaiacha.

Kama mtakumbuka ndiyo maana walikuwa wanasema wakati wa Mkapa hata bei za vitu zilikuwa zimetulia sana, zilikuwa hazirukiruki, ni kwa sababu tulikuwa tumejielekeza kwenye upande wa macro.

Sasa nini likuja kuvurugika mimi siwezi ku-



Waziri Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye

Inaendelea Uk. 14

Kona ya Dkt. Bisimba

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

TANZANIA imekuwa na bahati ya kuunganisha wananchi wake kwa lugha moja ya taifa; Kiswahili.

Inaelezwa kuwa Tanzania ina lugha za makabila yapatayo 120. Kama Kiswahili kisingekuzwa kufikia watu karibu nchi nzima, huenda ingekuwa kazi sana kuwasiliana kwa maendeleo yetu.

Julai 7 kila mwaka, tumeizoea kama siku ya Sabasaba. Lakini Novemba 2021 Baraza Kuu la UNESCO liliitaja tarehe hiyo kuwa ni Siku ya Kiswahili kupitia azimio lake namba 41 C/61.

UNESCO, ambalo ni shirika la Umoja wa Mataifa, likishughulika na masuala ya elimu, iliitaja siku hii kuwa ya Kiswahili kwa kutambua umuhimu mkubwa wa lugha hiyo.

Umuhimu huo ulibebwa na jukumu la lugha hiyo kukuza utamaduni anuwai, kujenga uelewa na kukuza mawasiliano baina ya watu na hata mataifa.

Maadhimisho ya kwanza yaliyofanyika mwaka 2022, yalikuwa na kauli mbiu isemayo; 'Kiswahili kwa Amani na Ustawi.'

Kila mwaka siku hii hupaswa kuadhimishwa kimataifa ili lugha hii itumike kama nguzo ya umoja, amani na kukuza utamaduni wa amani.

Maadhimisho hayo ya kwanza yalitumiwa kukuza uwezekano wa Kiswahili kuchangia kwenye maendeleo endelevu kimataifa ya 2030 na kwenye ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063: Afrika Tuitakayo.

Waliohudhuria maadhimisho hayo yaliyofanyika Paris, Ufaransa ambao walijumuisha wanataaluma, vijana na asasi za kijamii, walitoa uelewa wao wa njia za kukuza upekee wa Kiswahili katika utamaduni.

Mwaka huu maadhimisho hayo pia yalifanyika Paris kwenye makao makuu ya UNESCO yakiwa na kauli mbiu isemayo 'Kiswahili: Elimu na Utamaduni wa Amani.'

Aliyekuwa kiongozi katika maadhimisho hayo mwaka huu ni Balozi wa Congo huko Paris.

Nilipokuwa naangalia na kusikia haya nilijiuliza hivi sisi Watanzania ambao Kiswahili ndiyo lugha yetu kuu, tunafahamu kuhusu hii siku na umuhimu wake kwetu na kwa dunia kwa ujumla?

Tunafahamu kuwa Kiswahili ni kati ya lugha kumi zinazotumika sana ulimwenguni na ina wao ongeaji milioni 230?

Je, tunafahamu kuwa Julai 7 ilichaguliwa kuwa

Watanzania wanaifahamu Siku ya Kiswahili Kimataifa?



Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango (kulia), katika maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani. (Picha na Mtandao)

Siku ya Kiswahili kwa kukumbuka siku kama hiyo mwaka 1954 ambapo Mwalimu Julius Nyerere wakati wa uzinduzi wa TANU alikitangaza Kiswahili kuwa lugha rasmi itakayokuwa kama chombo cha kupigania uhuru?

Maswali hayo nimeyauliza kwa vile pamoja na kuwa Rais Samia Suluhu Hassan akipokea siku hii ilipoteuliwa alisema tumepata heshima kama nchi na tumependelewa kwa lugha yetu kuwa ya kwanza Afrika kutambulika hivyo.

Ukitazama ni miaka mitatu sasa siku hii inaadhimishwa kimataifa, lakini si kwa vyombo vya habari au hata kwa serikali na wananchi kuonekana kuiinua hii siku na kupokea fursa zinazopaswa kuja nazo.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

Ana kwa Ana

Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Inatoka Uk. 12

jua, mngewauliza sasa wale waliofuatia wangesema kiliharibikia wapi.

Pambazuko: Kwa kawaida nchi inaongozwa kwa kutumia Mpango wa Maendeleo wa Taifa, lakini hapa kwetu hakuna utaratibu wa kisheria kulinda mpango huo wa taifa. Unalionaje hili?

Sumaye: Ni kweli hilo tatizo na siyo la Tanzania tu, ni kwa Afrika nzima na ndiyo sababu kubwa ya Afrika kutokuwa na maendeleo endelevu na imekuwa kawaida.

Unakuta kuna mipango mizuri kabisa ya kitaifa, halafu anakuja mwingine anaiweka pembeni halafu anaanza yake mipya.

Mimi nakumbuka Mzee Mkapa wakati wa mkutano wa World Economic Forum uliofanyika Dar es Salaam, pale Mlimani City, alieleza bayana kabisa kwamba ukishatoka madarakani, hakuna mtu anayetaka tena kukutumia wala kukuuliza jambo lolote.

Na akasema kwamba; 'nataka niwaambie wenzu huko nje wanatufaidi sana na kututumia, lakini huku ndani sisi tunaonekana hatufai.'

Kwa hiyo, kuna hilo tatizo katika Afrika sijui tutalifanyeje na siyo awamu mmoja, ni karibu kila awamu ina tatizo hilo.

Pambazuko: Taasisi nyingi zilizopo hivi sasa mlizijenga na Mkapa, nini ilikuwa msingi wake?

Sumaye: Ni kweli tulijenga taasisi ili ziwe na nguvu kuliko watu, hasa viongozi, lakini baadaye zikaja kuyeyushwa mpaka sasa hivi huoni taasisi ambayo ina nguvu.

Kwa hiyo sasa hilo la kujenga taasisi ni kitu kimojawapo ambacho ukikaa unajivunia kwamba angalau nilisaidia nchi yangu kujenga hizi taasisi.

Sanasana kwa sababu bila taasisi zenye nguvu, hata kwenda kwenye uchumi wa ushindani huwezi kwenda, inakuwa ngumu, kwa hiyo hayo ndiyo matatizo yetu, lakini tuombe tu Mungu kwamba tutaendelea kujirekebisha taratibu.

Pambazuko: Pengine sasa ni wakati wa kuwa na Katiba mpya ili kuweka mifumo mizuri inayoongoza nchi?

Sumaye: Mimi kwangu hili swali nilishaulizwa

Inaendelea Uk. 15



Waziri Mkuu Mstaafu, Fredrick Sumaye, akizungumza na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Pambazuko, Peter Nyanje (kushoto) wakati wa mahojiano maalum na gazeti hili ofisini kwake jijini Dar es Salaam hivi karibuni. (Picha na Fidelis FELIX)



Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Inatoka Uk. 14

mara kadhaa na nilijibu kwamba sidhani kwamba kama Katiba mpya ni suluhisho la matatizo yetu yote.

Kwa lugha na nini ni tamu, lakini haiwezi ika-
zuia kiongozi mbaya kufanya mambo mabaya
kama hii mifumo tunayoisema haina uwezo wa
kumdhibiti.

Katiba tuliyokuwanayo hadi leo kimsingi,
ni Katiba ambayo ameitumia Mwalimu (Julius)
Nyerere, Mzee (Ali Hassan) Mwinyi, Mzee Mka-
pa na Jakaya Kikwete, lakini utawala wa (John) Ma-
gufuli ukawa kitu kitu kingine tofauti na tawala
zilizokuwepo na Katiba ni hiyohiyo.

Kwa hiyo watu wasije wakafikiri kwamba Kat-
iba ndiyo mwarobaini wa kila kitu.

Kinachotakiwa ni mifumo iliyo na nguvu. Ka-
tika nchi za wenzetu, mifumo inawekwa ambayo
ina nguvu, rais hawezi kuamua kufanya kitu am-
bacho ni cha ovyo, lazima mfumo utamzuia.

Hapa kwetu Tanzania rais anaweza kuamua
kufanya kitu cha ovyo akitaka na asifanywe kitu.

Hiyo ndiyo tofauti kubwa sisi na walioendelea.
Matumaini yangu ni labda tutafika huko, lakini
bila kufika huko tutapiga 'mark time' sana.

Pambazuko: Huoni kama Katiba mpya ingeku-
ja kuweka hiyo nguvu ya mifumo ili kuhakikisha
tunakwenda sawasawa?

Sumaye: Bado nasema Katiba mpya inaweza
kusaidia tu hapa na pale, lakini mifumo ni tofauti
kidogo.

Kinachotakiwa Katiba iendane na mifumo
kwa utendaji zaidi.

Kwa mfano, Marekani, rais wake hawezi kufa-
nya kitu chochote kikubwa bila system (mfumo)
kukubali na akitaka kufanya itamzuia na kum-
dhibiti na hana la kufanya.

Pambazuko: Wewe ni waziri mkuu uliyehu-
dumu kwa muda mrefu kuliko mawaziri wakuu
wengine, ni kitu gani hasa unachojivunia kwamba
uliweka nguvu na hata leo unaweza kujipiga kifua
kwa mafanikio?



Benjamini Mka-
pa

Sumaye: Asante sana, hilo ni swali ambalo
nimeulizwa mara nyingi, lakini kwangu huwa ha-
lina maana sana kwa sababu kama ukijua kazi za
waziri mkuu.

Kama wakati huo mambo yalikuwenda vizuri,
basi ujue waziri mkuu ndiye alikuwa mtendaji
mkuu wa serikali. Kwa hiyo kusema mimi nianze
kunyofoa niseme kitu fulani nilifanya, huo ni ud-
haifu wa utawala na ubinafsi.

Kwa sababu mimi naweza kukwambia kwam-
ba katika kipindi tulichoingia madarakani uchumi
ulikuwa mgumu sana.

Tumesimamia uchumi hadi ukasimama uka-
wa mzuri hadi majirani zetu wakawa wanatuogopa,
lakini siyo hilo tu, tumesimamia pia ukuaji wa
demokrasia, mimi ndiye nilikuwa waziri mkuu
wa kwanza wa bunge la vyama vingi.

Kwa hiyo, tumeisimamia demokrasia na tu-
meiacha demokrasia ikiwa inakua vizuri na ina
nguvu, tumefanya mambo mengi tu, nikienda
kwenye elimu, afya na mambo mengine mengi,
ndiyo kazi ya waziri mkuu.

Bunge lilikuwa na nguvu kubwa sana kama

Inaendelea Uk. 18

Habari

Raha, raha zaidi na karaha za treni ya SGR

Na Waandishi WETU,
Dar es Salaam - Morogoro

MWEZI uliopita - Juni, 2024, Tanzania iliingia katika historia ya kuwa nchi ya kwanza katika eneo la Afrika Mashariki na Kati kuwa na treni ya umeme katika reli ya kisasa (SGR).

Historia hiyo iliandikwa baada ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), lilipoanza safari za abiria kati ya Dar es Salaam na Morogoro.

Mengi yaliandikwa na abiria na watu wengine waliotumia usafiri huo kuhusiana na waliyoshuhudia wakati wakisafiri.

Pambazuko halikutaka kuwa nyuma, nalo likaamua kutuma waandishi wake kushuhudia moja kwa moja kilichopo kupitia usafiri huo.

Waandishi wa Pambazuko wakafanya safari kutoka Dar es Salaam kuelekea Morogoro na kurudi kwa kutumia treni hiyo.

Mengi mazuri, ya kuvutia na kusifu yanashuhudiwa na waandishi wa Pambazuko na kwamba treni hii ya SGR ni moja ya hatua kubwa ya maendeleo ambayo Tanzania imewahi kufanya.

Ni aina ya usafiri ambao Tanzania na watu

wake, wanapaswa kujivunia kwa sababu kuna dalili zote kuwa utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi.

Ni usafiri wa haraka, ni wa starehe, ni wa ki-staarabu, ni wa kisasa, ni kielelezo cha kweli cha maana ya usafiri wenye tija na ufanisi uliopangiliwa vizuri.

Moja kati ya matatizo mengi ya sifa za Watanzania, ni kutozingatia muda, lakini hilo halipo kwa treni za SGR.

Muda ambao umeandikwa kwenye tiketi wa kuondoka na kufika, ni muda ambao kweli safari itaanza na kumalizika.

Mkiwa safarini, kama unatumia treni ya kawaida, ukitangaziwa kuwa treni itasimama kituoni kwa muda wa dakika mbili, basi ni kweli itakuwa hivyo.

Wahudumu ndani ya treni wako maridadi, wakiwa na nyuso zenye tabasamu na bashasha.

Taarifa imetolewa wiki iliyopita inasema kuwa treni hiyo inabeba jumla ya abiria 4,000 kila siku kwa safari zake za Dar es Salaam hadi Morogoro.

Inatarajiwa kuwa idadi ya abiria itaendelea kuongezeka pale safari za Dodoma zitakapoanza mwishoni mwa mwezi huu.

Lakini, kati ya raha hizo za usafiri wa treni ya SGR, kuna karaha zake chache na Pambazuko imeona ni vyema kuzibainisha ili kuwa njia ya kushauri marekebisho ambayo yataufanya usafiri huu kuwa bora zaidi.

Kumbi za abiria kusubiria usafiri

Inaendelea Uk. 17



Abiria wakisubiria treni ya umeme katika kituo cha Dar es Salaam hivi karibuni. (Picha na Fidelis FELIX)



Raha, raha zaidi na karaha za treni ya SGR



Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa

Inatoka Uk. 16

Moja ya kasoro kubwa ambazo waandishi wa Pambazuko wamezibaini ni ufinyu wa maeneo ya abiria kukaa wakati wakisubiri muda wa kuanza safari.

Hilo limebainika katika vituo viwili vikubwa; Dar es Salaam na Morogoro.

Waandishi wa Pambazuko walisafiri kwa treni iliyokuwa na jumla ya mabehewa 14, mengi yakiwa ni yale ya daraja la kawaida ambayo yanachukua abiria 78.

Kwa hesabu, kama nusu ya mabehewa haya 14 yatakuwa ni kwa ajili ya abiria wa daraja la kawaida, basi treni hiyo itakuwa na zaidi ya watu 500.

Lakini katika vituo vya Dar es Salaam na Morogoro Pambazuko limeshuhudia idadi ya viti katika maeneo ya abiria kusubiria haifiki 200.

Ni vichache ikilinganishwa na idadi ya watu wanaosibiri kupanda treni.

Hali ilikuwa tete kidogo wakati wa safari ya kurejea kutoka Morogoro ambapo watu zaidi ya 500 walilazimika kusimama kwa kubinyana katika kituo cha Morogoro kwa sababu eneo la kusubiria ni finyu sana.

Vyumba vya VIP

Kwenye vyumba kwa ajili ya watu maalum (VIP), Pambazuko limeshuhudia kukiwa kumejaa maboksi.

Yupo abiria mmoja ambaye alikata tiketi ya daraja la juu ambaye alipaswa kusubiria treni

kwenye chumba hicho, lakini kutokana na kuba-dilishiwa matumizi, alilazimika kukaa na abiria wa daraja la kawaida.

Huduma muhimu vituoni

Hili nalo siyo tatizo kubwa, lakini inapaswa litafutiwe ufumbuzi haraka.

Mpaka wakati safari za treni hii zinaanza, inaonekana kuwa shirika na wadau wake, walikuwa hawajajipanga kutoa huduma muhimu katika vituo.

Katika vituo, hakuna huduma muhimu kama vile maduka, huduma za kibenki, kampuni za simu, migahawa na vituo vya huduma za kwanza kwa kutaja huduma chache.

Pambazuko linatambua kuwa TRC imetoa fursa kwa wafanyabiashara wengine kuwekeza katika maeneo hayo na wawekezaji ndio wamechelewa.

Kuna umuhimu wa TRC kuhakikisha huduma hizo zinapatikana haraka kwa sababu kasoro yoyote ambayo abiria wataiona, wanaihusisha moja kwa moja na TRC.

Elimu kwa abiria

Upo umuhimu wa kutoa elimu kwa abiria kuhusu namna ya kutumia ama kufuata maelekezo yanayotolewa kwa ajili ya abiria.

Kuna vibao vingi vinavyoelekeza abiria akae wapi, asubiri wapi kabla ya treni kuwasili, lakini kuna changamoto kwa baadhi ya abiria kufuata.

Tatizo ni kuwa kwa Watanzania wengi huu ni usafiri 'mpya' na matumizi ya miundombinu mingi ni suala geni kwao.

Pamoja na ishara za maelekezo yanayopatikana kwenye vibao na hata wakati mwingine kutangazwa, bado kuna abiria kadhaa wanaobabaiika na wasijue wafanye nini.

Ni dhahiri kuwa TRC inabidi ichukue hatua za ziada kuhakikisha abiria wanaeleweshwa zaidi kuhusu wanayopaswa kufuata wanapokuwa wakisafiri kwa treni ya kisasa.

Mathalan, katika kituo cha Dar es Salaam, kuna miundombinu kama vile ngazi za umeme (escalator) ambazo watu wengi hawajui jinsi ya kuzitumia.

Inaendelea Uk. 22

Ana kwa Ana

Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Inatoka Uk. 15

mnakumbuka, lilikuwa Bunge kwelikweli, lakini waziri mkuu ndiye mkuu wa shughuli za serikali bungeni.

Hizo reform (mageuzi) zote ninazokueleza tu-lifanya civil service reform (mageuzi ya utumishi wa umma, bila kuwepo vurugu na mara nyingi wenzetu huko nje wanashangaa tumewezaje ku-fanya mageuzi makubwa hivyo bila nchi kuingia kwenye vurugu.

Pambazuko: Mzee Mkapa aliandika kitabu ambacho kinasaidia watu kujifunza. Je, wewe una mpango kama huo?

Sumaye: Huo mpango ninao ila bado sijaanza.

Pambazuko: Na unaionaje hali ya demokrasi hivi sasa nchini kwa sababu wewe ulikuwa CCM ukaenda upinzani, ukarudi tena CCM. Unadhani demokrasia inakua?

Sumaye: Actually (kwa kweli) kwa upande wa demokrasia, mimi nilipokwenda upinzani na nilieleza vizuri sana kwenye kikao changu na waandishi wa habari.

Nilisema siendi huko labda kwa sababu nina hasira na CCM au nina hasira na mwenyekiti ambaye alikuwa Kikwete au nina hasira na aliyeteuliwa ambaye ni Magufuli, nikasema la hashia!

Lakini kitu ambacho kilinipeleka kule na hadi leo ninaamini hivyo na niliporudi CCM nilikisema, ni kwamba kama tuko kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, ni hatari sana kwa usalama wa nchi kwa chama kimoja kuwa tu kikubwa na vingine vikawa vidogo kabisa havina maana.

Kwa sababu katika mfumo wa vyama vingi iko siku watu watafikataa chama hiki na nikatumia neno hili nikasema; hata kama chama hicho kinafanya vizuri kama malaika, watu kuna siku itafika watafikataa.

Watakapokikataa kama kule upande wa pili hakuna mwenye uwezo wa kubeba nchi, nchi itaingia kwenye vurugu.



Rais mstaafu Benjamin Mkapa (kushoto), akisalimina na Waziri Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye.

Nikasema mimi nahama na kuhama kwangu CCM itafadika zaidi kwa sababu itakuwa macho zaidi.

Lakini nahama kwa lengo la upande wa pili uwe na nguvu ili siku ambayo watu watasema sasa kuna mabadiliko, angalau nchi isiangukie kwenye mikono ya watu wasio na uwezo kabisa hii ndiyo ilikuwa sababu.

Na siku niliporudi na nilipopokelewa nili-waeleza nikasema na bado nasema hata ndani ya CCM kwamba CCM inahitaji chama cha upinza-ni chenye nguvu, ili iweze kushindana.

Lakini kama mambo yatashindikana, basi nchi isiangukie mikononi mwa watu wasio na uwezo kabisa.

Nilisema pia kwa bahati mbaya, kwa vyama vilivyopo, sioni chama ambacho kinaweza kika-jijenga kikawa chenye nguvu, inabidi vijana au watu wengine ambao ni wanasiasa proper (sahi-hi), wajenge vyama vya upinzani.

Sasa tunapokuwa na vyama vyenye nguvu, ndiyo tunaweza kupata vyama vinavyoweza kushindana na CCM kisiasa na siyo kiuharakati.

Nimefanya kazi kubwa sana ndani Chadema. Nikagundua kwamba sifiki popote, badala yake ninakuwa sieleweki na wakaanza tu kusema ooh huyu bwana ametumwa na CCM, hivi mimi mtu mzima natumwaje na CCM?

Inaendelea Uk. 25

Mifumo yachochea migomo kwa wafanyabiashara



*Wafanya-
biashara
wa soko la
kimataifa
la Kariakoo
wakiwa
wamefunga
maduka
kufuatia
mgomo
uliotokea
hivi kari-
buni. (Picha
na DW)*

Na Aloysius MUJULIZI

MINYUKANO kati ya serikali na wafanya-biashara nchini Tanzania, imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Zipo sababu nyingi zinazoelezwa kuwa chanzo, lakini kwa utafiti wa haraka, sababu kubwa ni kuwepo kwa mifumo inayosababisha hali hiyo.

Kwamba kuna mifumo ambayo haina afya kwa watu wake wanaopaswa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo.

Inavyoonekana, mifumo iko kwenye kupendelea serikali zaidi, huku mfanyabiashara akisahaulika.

Mifumo iliyopo, inatoa mwanya wa kuibuliwa kwa maswali mengi, lakini yanakosa majibu.

Maswali hayo ni pamoja na kwamba ni lini wafanyabiashara wetu wamejifunza utamaduni wa kutunza vitabu vya biashara hata kulipa kodi stahiki?

Je, ni lini serikali kuu na serikali za mitaa zimeweza kulea, kukuza na kuwezesha ukuaji wa biashara na wafanyabiashara?

Ni lini serikali imeandaa watendaji na

utendaji rafiki kwa biashara? Sambamba na kuandaa utaratibu muafaka na mifumo rahisi ya ukusanyaji wa kodi?

Tujiulize, hivi mlipakodi ni nani? Maana ipo taswira isiyo sahihi ya kwamba mlipa kodi ni mfanyabiashara. Hili linatunyima fursa ya kutatua tatizo sugu kuhusu sera zetu kuhusu biashara.

Uhalisia ni kwamba, mlipakodi ni mzalishaji na mlaji wa bidhaa, huduma au mazao.

Tuchukue mfano wa mkulima wa kahawa. Tumfanye awe mwana ushirika. Atakatwa kodi kwa kuuza mazao, kwa kununua pembejeo na hatimaye kodi ya mapato.

Lakini pia akinunua chumvi, sukari, nguo, mafuta ya kupikia na hata akiamua kuburudika kwa kunywa soda au kilevi pia analipa kodi.

Kwa mfano huo, ushirika ni mkusanyaji kodi tu kwa niaba ya serikali. Hivyohivyo kwa mfanyakazi, mwajiri ni mkusanya kodi kwa niaba ya serikali.

Lakini linapokuja suala la mfanyabiashara yeye anavaa wajibu wa mlipakodi, sambamba na wakazi wengine ndani ya nchi. Lakini pia anabe-

Inaendelea Uk. 23



Makala

Serikali inayaona na kuyaelewa maandishi haya ukutani?

Rais Samia Suluhu Hassan

**Na Mwandishi WETU,
Dar es Salaam**

KATIKA kitabu cha Daniel ndani ya Biblia kuna simulizi ya Nabii Daniel inayohusu kiganja cha mkono kilichoandika maandishi kwenye ukuta wa jumba la Mfalme Belshaza.

Mfalme na watu wake walipata shida sana kutambua maana ya maneno yale na ndipo Mfalme akaamuru Nabii Daniel aletwe kutoa tafsiri. Mfalme alimtaka Daniel afanye hivyo kwa sababu alishajipambanua kuwa mfasiri maono.

Daniel alitoa maana ya maneno yale ya Mene, Mene, Tekeli, na Peresi.

Kuna mambo yanatokea leo hii unaweza kuyalinganisha na maandishi katika ukuta wa Mfalme Belshaza kwa serikali yetu. Na kwa mfanano inaonekana kana kwamba serikali na waliomo ndani yake bado hawajatambua maana yake kama ilivyokuwa kwa Mfalme Belshaza.

Ingawa, kuna uwezekano mkubwa kuwa wapo miongoni mwao wanatambua maana ya maneno

haya lakini kwa sababu akili zao zimezibwa aidha na woga au tamaa, wameamua kujifanya hawayalewi mandiko hayo na hivyo kuifanya serikali nayo ionekane haitambui maana ya maandishi hayo.

Katika miaka ya hivi karibuni imeibuka tabia ya watu wengi katika jamii kuonyesha hisia za huruma wenzao ambao wameingia matatizoni na serikali. Huruma ya watu hawa inaonekana kupitia jinsi wanavyowasaidia hao walioingia matatizoni na serikali.

Mfano wa hivi karibuni ni tukio la kijana mmoja huko Mbeya kuchangiwa zaidi ya shilingi milioni tano zilizomwezesha kulipa faini baada ya kutiwa hatiani kwa makosa ya mtandaoni.

Kijana huyo, Shadrack Chaula, alihukumiwa kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya shilingi milioni tano baada ya kutiwa hatiano na mahakama aliposhtakiwa kwa kitendo chake cha kuichoma moto picha ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali kabla kesi hiyo haijasikilizwa, katika

Inaendelea Uk. 21

Serikali inayaona na kuyaelewa maandishi haya ukutani?



Edgar Mwakabela, maarufu Sativa

Inatoka Uk. 20

moja ya hotuba zake, Rais Samia alionyesha kuchukizwa na kitendo kilichofanywa na kijana huyo. Na pengine ni kutokana na kauli hiyo, kijana huyo alikamatwa na kushitakiwa kwa haraka. Kesi yake ni moja ya kesi ambazo zimevunja rekodi ya kusikiliza kwa kasi ya ajabu.

Siku ambayo Chaula, kijana msanii wa uchoraji, aliyofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Run-gwe mkoani Mbeya, siku hiyo hiyo kesi ilisikilizwa na kukamilika na hukumu ikatolewa siku hiyo. Hii ni rekodi ya aina yake katika nchi ambayo kesi nyingine huchukua miaka kadhaa kabla hazi-jaanza kusikilizwa.

Kimsingi huyu ni mhalifu, tena aliyekiri kosa mahakamani na kuhukumiwa. Ilitarajiwa kuwa wengi katika jamii wasimuonee huruma lakini kili-chotokea na kinyume chake.

Jamii haikumchukulia kama mhalifu, bali mtu aliyeonewa na hivyo ikaamua kumsaidia.

Ukatolewa wito wa watu kuchanga ili kupata fedha zitakatumika kumlipia faini kijana huyo ili aepukane na kifungo. Katika kipindi cha saa kadhaa tu michango iliendeshwa nchi nzima na kiasi cha alichopaswa kulipa faini kikapatikana. Kwa kuwa ilikuwa ni mwisho wa wiki ambapo taasisi za serikali hazifanyi kazi basi ilipofika siku ya kazi watu wakaenda kulipa faini hiyo na kijana huyo kuachiwa.

Baadaye amwakili wabobevu nchini wakatan-

gaza azma yao ya kumsaidia kijana huyo kukata rufaa.

Hapo kabla tulimeshuhudia matukio mengi ya watu walioingia matatizoni, hasa matatizo yao ya kionekana kuwa na mkono wa serikali, hata kwa hisia tu, jamii huwaonea huruma na kuwasaidia.

Walimchangia Tundu Lisu alipopigwa risasi na kupelekwa Ulaya kwenye matibabu, wengi aki- amini kwua swerikali ilikua na mko no kwenye shambilizi dhidi ya mwanasiasa huyo. Wakam- changia tena Lissu alipokabidhiwa gari lake na polisi. Watu wengi walimtaka aliweke gari hilo makumbusho kama kumbukumbu ya tukio la yeye kushambuliwa kwa risasi. Lisu akasena alitamani kufanya hivyo lakini inabidi alikarabati ili aendelee kulitumia kwa kuwa hana gari jingine.

Wananzengo wakamwambia asipate shida, wakaanzisha michango ili kumwezesha kununua gari jingine ili ile azma ya kuliweka gari hilo ma- kumbusho itimie.

Edgar Mwakabela, maarufu kama Sativa, ali- poonekana akiwa amejeruhiwa vibaya ua kutup- wa porini huko Katavi baada ya kupotea kwa siku kadhaa, watu wakajitokeza kumchangia fedha na wakafanikiwa kumsafirisha kutoka Katavi hadi Dar es Salaam ambako alifikishwa kwenye hospitali ya hadhi ya kubwa Aga Khan.

Zipo taarifa kuwa familia ya Sativa ilikataa fed- ha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kugharamia matibabu ya kijana wao, wakidai si busara kwa ser- ikali kutoa fedha za matibabu bila kuonyesha jiti- hada zozote za wazi kuwapata watu waliohusika kumteka, kumtesa na kumuumiza Sativa.


Haya ni kati ya matukio mengi ya aina hii am- bayo yanatoa maswali mengi kwa mtu wa kawaida.

Matukio kama haya yanaweza kuwa ni sawa na yale maandishi ya kiganja kwenye hadithi ya Nabii Daniel na Mfalme Belshaza.

Sijui kama serikali inajiuliza ni jambo gani linaifanya jamii iwe na huruma na atu ambao wa- naonekana kuingia matatizoni na serikali?

Katika baadhi ya matukio, hata mtu aliyetiwa hatiani kwa kukiri kosa bado jamii inaonekana kuwa na huruma naye. Sijui kama serikali inajiuli- za kulikoni? Hali hii inasababishwa na nini?

Hivi Daniel wa serikali ni nani awatafsirie maan- dishi haya ambayo tunayaona kupitia matukio kad- haa siku za hivi karibuni?



Raha, raha zaidi na karaha za treni ya SGR

Inatoka Uk. 17

Eneo hilo linahitaji watu mahsusi wa kutoa 'elimu' kwa abiria ili kuwawezesha kuitumia miundombinu huyo kwa usalama zaidi.

Wapo ambao wanapata shida kupanda kwenye ngazi hizo ambazo hutembea zenyewe. Na wakifanikiwa kupanda basi, kwenye kushuka nako kunakuwa na "shughuli nyingine" kiasi kuwa wengi huanguka na kuumia.

Ndani ya treni

Kama inavyofahamika kuwa treni hii ni mpya na kila kitu kilichomp ni kinavutia, lakini kwa upande wa huduma ni muhimu TRC ikafikiria kuboresha huduma za burudani kwani 'screen' iliyopo inatumika kutoa matangazo ya TRC pekee.

Ni vyema pamoja na matangazo hayo, kukawepo burudani nyingine pia zinazoonyesha au hata kuwepo kwa habari muhimu.

Pia, kwa kuwa abiria hawaruhusiwi kuingia na vyakula ilikuwa ni matarajio ya Pambazuko kuwa huduma hizo zitapatikana kwa wingi na kwa haraka ndani ya treni.

Lakini, katika safari ya kwenda, waandishi wetu hawakupata huduma za staftahi ndani ya treni kwa sababu abiria wanazuiliwa kuzungukazunguka ndani ya treni.

Na katika safari ya kurudi, hata viburudisho kama soda havikuwepo, licha ya watu kuwa na pesa wakihitaji huduma hizo.

Pia hakuna huduma za kuridhisha kwa watu ambao wangependa kubebewa mizigo wakati wa kuingia na kushuka kwenye treni.

Hakuna matoroli mahsusi ya kubebea mizigo, hivyo abiria wanlazimika kubeba mizigo yao aidha kichwani au mikononi.

Kwa upande wa unadhifu wa watoa huduma, Pambazuko limefurahi kuona wale wahudumu wa TRC wakiwa nadhifu katika sare zao zinazopendeza.

Upande wa watoa huduma wengine, kama vile wanaofanya usafi, ambao tunaamini ni kampuni iliyopewa kandarasi na TRC, wafanyakazi wake hawana sare maalum na hivyo kuleta

picha isiyofurahisha.

Miundombinu kuja kwenye kituo

Pamoja na kwamba TRC haihusiki moja kwa moja, lakini ni jambo jema kwa shirika hilo kuweka msukumo kwa wawekezaji wengine kuweka miundombinu inayoelekea kwenye treni hiyo.

Pale Morogoro, barabara kuja kwenye kituo cha reli ni mbaya na ina vumbi jingi.

Barabara hiyo hailingani hata kidogo na 'usa-sa' unaopatikana kwenye treni ya SGR.

Kongole

Wafanyabiashara ya usafirishaji waliozungumza na Pambazuko kituoni Morogoro, wanaishukuru TRC kwa kuanzisha usafiri huo kwani umeinua kidogo biashara zao.

Wanaamini mambo "yatakapochanganya," basi na wao hali itakuwa nzuri kidogo upande wao.

Ni vyema sasa kuungana na wito uliotolewa na Mkurugenzi wa TRC, Masanja Kadogosa wakati akizungumza na vyombo vya habari, akiwataka Watanzania kutunza miundombinu ya reli.

Huu ni uwekezaji muhimu na mkubwa, uliogharimu taifa fedha nyingi. Pamoja na kuwa ndio kwanza unaanza kutumika, lakini umeonyesha kuwa utaleta mapinduzi makubwa kati ka sekta ya uchumi, usafiri na usafirishaji.

Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha uwekezaji huu unalindwa na kutunzwa kwa ajili ya manufaa ya kizazi hiki na kizazi kijacho.

Kadogosa anasema kuwa reli hii imeundwa kudumu kwa kipindi cha miaka 100, lakini kudumu huko kutatarajia kwa kiasi kikubwa, jinsi miundombinu ya reli hii itakavyotunzwa.

Tuitunze miundombinu hii ili tuje tuwarithishe wajukuu zetu kama vile ambavyo mababu zetu wameturithisha reli ile ya zamani ya MGR.



Je wajua



Binadamu huzaliwa na mifupa 300, lakini mpaka anapokuwa mtu mzima anakuwa amebaki na mifupa 206 tu.

Kinachosababisha mifupa ipungue ni baadhi ya mifupa huungana na kutengeneza mfupa mmoja.



Bangi husababisha macho kuwa mekundu kwa sababu ya 'Cannabinoids' ambazo huenda na kujishikiza kwenye 'receptor' kitendo kinachosababisha damu kusafiri kwa wingi katika macho.

Mifumo yachochea migomo...

Inatoka Uk. 19

ba wajibu wa kukusanya kodi kwa niaba ya serikali.

Kwa hiyo mzigo huo wa kukusanya kodi ya serikali anaubeba mara mbili; moja kwa kulipia kodi ya forodha na tozo za kuingiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Hili analifanya kwa kuwakopesha walaji watarajiwa; yaani wateja wake, ambao wanalipia kupitia bei ya bidhaa. Lakini anabeba hasara pale ambapo bidhaa hiyo isiponunuliwa.

Mzigo wa pili ni kwa kodi za ulaji - tozo za ndani kwenye bidhaa. Na hapa ndipo palipo na changamoto kubwa.

Mfanyabisahara akiwa mwaminifu kabisa ina maana atalipia kodi kubwa kwenye mapato. Yaani kodi juu ya faida.

Hapa Tanzania ni asilimia 30 bila kubagua ukubwa au uchanga wa biashara. Hii ndiyo inayozaa biashara ya bei tofauti 'ukitaka au usipotaka' kuchukua risiti.

Tukumbuke ule mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (Mkurabita) pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (Mkukuta) ulilenga kuishawishi jamii yetu - walaji na wafanyabiashara - kuupokea, kuuzoea na kuukubali utamaduni wa kurasimisha mienendo na tarati bu zetu.

Rahisi ni aghali

Nionavyo mimi kuna haja ya kutoka kwenye sera za kukusanya viwango fulani vya mapato ya kukidhi matumizi, badala yake tuwekeze zaidi katika kupanua uzalishaji. Kwa maana ya wigo wa kodi.

Kukuza biashara na ufa-nyaji wa biashara kwa nchi yenye lango la bahari ni suala nyeti na muhimu.

Maana utaachaje soko la 'Mtakuja' ambapo una ushindani unaojulikana wa bandari na usafirishaji kwa nchi jirani halafu ukaingia kwenye soko la wote na lisilotabirika?

Ukiwasikiliza wafanya-biashara wa Kariakoo, Dar es Salaam huwezi kukosa kushangaa? Yaani tunafukuza wateja, huku tukijenga na kupanua bandari, reli na barabara.

Kwa nini tunachukia biashara na wafanyabiashara? Ni lini nchi yetu itarejea kuwa ya wote na isiwe ya wakulima na wafanyakazi tu?

Inakuwaje mataifa mado-go - visiwa kama Uingereza, Singapore, Hong Kong, ambako hakuna rasilimali kama madini, ardhi kubwa, misitu, lakini kuna ustawi mkubwa wa biashara na sisi wenye soko - tena na majirani wengi wasiokuwa na bandari, tuka-wa ni wenye kuipiga vita biashara?

Mujulizi ni mwanashaeria anayepatikana kupitia email hii: ask.mujulizij@mrmattorneys.co.tz



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Ole wenu ninyi wabunge mliotutelekeza

MWISHONI mwa mwezi Juni mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliahirisha Bunge la Bajeti jijini Dodoma.

Kwa kawaida Bunge, hasa la bajeti, linapohirishwa, baadhi ya wabunge hujawa furaha ya kuondoka jijini Dodoma ili wakaungane na familia zao ambazo wamekuwa nazo mbali kwa takribani miezi mitatu ya kuhudhuria vikao.

Wakati huohuo, wabunge wengine wanakuwa na hamu ya kurudi majimboni kwao ili wakapate muda wa kushirikiana na wapigakura wao katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Lakini, kwa kuwa kuna baadhi ya wabunge ambao wamekuwepo kwa miaka mingi, hawataki kurudi majimboni baada ya kuahirishwa kwa Bunge.

Sasa basi, hapa nafanya kuwakumbusha wabunge hawa ili wananchi watakapochachamaa na kuwakataa, wasije wakamlaumu mtu.

Baadhi ya wabunge hao hawana muda na majimbo yao, hawataki kusaidia ujenzi wa barabara, hawataki kuboresha huduma za afya, elimu na maji majimboni kwao. Wengine hawataki hata kukanyaga jimboni.

Wao hutumia muda mwingi kufanya mambo yao binafsi, bila kujali kuwa kama siyo kura wasingeweza kuyafanya mambo hayo.

Wabunge hao hawataki hata kupokea simu za wapigakura wao, hawataki kusikia shida zinazoletwa na wananchi wa majimbo yao, bali wao wanatumia muda wao mwingi kula raha na kushughulikia biashara zao.

Kwa hiyo basi, nawaambia wabunge hao, kwamba ole wenu nyinyi mnaojiona wa maana zaidi kuliko wananchi waliowawezesha kuwa madarakani kuanzia mwaka 2020 hadi sasa, kwa sababu hamjui mnachokifanya.

Nawaambia tena ole wenu kwa sababu wapigakura katika majimbo yenu wanawaangalia kwa jicho la huruma kwani itakapofika mwakani, wakati mtakapokwenda kuwaomba ridhaa ya kuendelea kukaa kwenye raha, nao watajua wawaadhibu vipi kwa kuwa mmewaonyesha dharau tangu walipowachagua miaka minne iliyopita.

Nasema msije mkamtafuta mchawi pindi wananchi watakapowakataa majimboni kwenu.

Lazima mtambue kuwa dharau mnazowaonyesha wapigakura wenu, ndizo zitakayokuwa chanzo cha nyinyi kutochaguliwa pindi uchaguzi mkuu utakapofanyika mwaka ujao.

Eleweni kuwa wananchi majimboni kwenu wanazo akili za kutosha, wanawaangilia utadhani hawawaangalii, wanawaona kama hawani, lakini utakapofika wakati wa nyinyi kusimama mbele zao na kuwaomba kura, hapo ndipo mtakapojua nguvu walizonazo wapigakura kupitia kura zao.

Wapigakura wenu hawatanunulika kwa vitenge, hawatashawishika kwa kanga, kofia na chumvi, ila wananchi hao watakuwa na uamuzi mmoja wa kuwanyima kura ili mkaendeleo na maisha mengine baada ya kuondoka madarakani.

Hakika nawaambia tena, ole wenu nyinyi wabunge mnaojisahau, na kuwaona wananchi kuwa ni kama takataka, baada ya kuwa mmeingia bungeni.

Nasema tena, ole wenu, endapo hamtawajali waliowapigia kura sasa, na kuanza kujipitisha uchaguzi ukikaribia, safari hii wapigakura wamejanjaruka. Mtakwama.

Jirekebisheni haraka.





Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Inatoka Uk. 18

Mimi nawafundisha siasa, nikawaambia mimi sijatumwa na CCM, nina nia njema, hiki chama tukibadilishe kiwe chama cha siasa, kisiwe cha uharakati kikiwa cha uharakati hatuwezi kuingia Ikulu.

Nikawaambia labda someni vitabu vyote vya ulimwengu huu, hakuna chama kinachoingia Ikulu wakati kinapambana na police force (Jeshi la Polisi), kinapambana na usalama wa taifa, kinapambana na nani... huwezi kuingia Ikulu, labda uwe na jeshi.

Kwa hiyo nilipofikia hatua hiyo nikasema ili chama kibandikike lazima tubadili uongozi, hapo ndiyo nilipogusa mboni ya jicho (anacheka) na shida ikaanzia hapo na ilikuwa kubwa mengine hata siwezi kueleza.

Pambazuko: Kwa hiyo unadhani kwamba changamoto kubwa ya vyama vya upinzani ni uongozi?

Sumaye: Kabisa kabisa. Watu hawataki kua-chia (uongozi) na vyama vinakuwa kama mali fulani ya mtu, ukishafikia hapo, hakuna chama cha siasa.

Chama cha siasa kama upo kwenye mfu-mo wa vyama vingi vyenye demokrasia, lazima demokrasia iwepo ndani ya chama.

Pambazuko: Samia ametimiza miaka mitatu na ushei madarakani, tumeshaona mambo anayoyafanya - unauonaje uongozi wake?

Sumaye: To be frank (niwe mkweli), mama Samia, mimi kwanza ninampenda kwa jinsi ambavyo anaendesha nchi bila makeke, lakini pia amerudisha matumaini ya Watanzania yaliyokuwa yamepotea.

Unajua watu hawaelewi... uelewa wa Watan-zania ni tofauti kubwa sana. Kuna watu walikuwa wanaona na wanasema Magufuli alikuwa anapeleka nchi kunakotakiwa.

Lakini watu wenye akili zao walikuwa wanao-na nchi inazama kabisa.

Mimi nilikuwa najua nchi inazama, na ilikuwa



imeshafika mwisho kabisa, mama Samia angalau ameirudisha (nchi) katikati kwenye usalama.

Sasa katika hilo kwa kweli mimi nina matumaini makubwa, kila mtu ana matatizo yake, hakuna aliyekamilika, hapa na pale najua wanamsema kwa hili na lile, lakini mimi nasema generally (kwa jumla) kama nchi ukiangalia ana-koipelekea, ni salama.

Sasa speed (kasi) ya kwenda inategemea na mambo mengi, lakini angalau direction (mwelekeo) unaiona. Leo hakuna mfanyabiashara ambaye anaogopa kufanya biashara kwa sababu mali yake itanyang'anywa.

Watu wa kodi wanafanya vituko hapa na pale, lakini pia anawaonya, ni tofauti na huko tulikotoka.

Kwa hiyo mimi nasema anaenda vizuri, watu wana amani, wanafanya kazi zao vyema, kuna mambo ya hapa na pale ambayo unaweza kusema labda hilo liko hivi, lakini kwenye utawala haya-kosekani.

Swali: Unadhani nini kifanyike ili Zanzibar iwe na utulivu kisiasa, kwa sababu tulidhani Serikali ya Umoja wa Kitaifa ingeweza kusaidia lakini bado. Hivi karibuni tu tumesikia tena ACT-Wazalendo wametishia kujitoa kwenye GNU?

Sumaye: Mimi ukiniuliza kuhusu Zanzi-



Ana kwa Ana

Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Inatoka Uk. 25

bar hivi sasa nitakwambia Zanzibari iko stable (imara) kuliko ilivyokuwa awali.

Ilikuwa na hali ngumu sana, tulikuwa tunaliangalia yai ambalo kila wakati utasema uweke nguo chini yake maana litadondoka.

Kuna maeneo wanayotakiwa kuyarekebisha, na wote wanatakiwa kukaa pamoja ili kujenga uaminifu na kupigania maendeleo kwa pamoja.

Ile ya "the winner takes all" (mshindi kwa kura nyingi kuchukua mamlaka yote) ilikuwa imefikisha Zanzibar pagumu sana, hata hivyo ilikuwa inapona kwa sababu iko kwenye Muungano, ingekuwa wao wenyewe wangeshapasua siku nyingi.

Kwa hiyo, hapo tulipo siyo pabaya, kinachotakiwa tu wakae chini tena, maana Katiba inatengenezwa kwa kuangalia mazingira yaliyopo sasa, nay ale ya huko mbele.

Sasa ukienda huko ukatumia hiyo Katiba kwa muda, ukaona kuna upungufu mahali fulani na inahitaji marekebisho, inatakiwa urekebishe using'ang'anie tu kuwa tumeshaitunga.

Kwa hiyo, kinachotakiwa tu ni hiyo ifanyike, lakini mimi naona Zanzibar sasa hivi hali siyo mbaya sana. Unajua ACT... usisahau kuwa ni CUF yaani (anacheka) ni ile CUF ya zamani ikawa ACT, kwa sababu technically (kiufundi) CUF ilifanywa isiwe chama hai kwa hiyo ili wasife wakajibadilisha kuwa ACT lakini ni CUF.

Sasa siasa ya CUF na CCM actually (kwa hakika) ni siasa za Afro Shiraz Party na Hizbu. Sasa wale watu hawaivi kabisa, unaweza kusema si vyama vya siasa, ni makundi vyenye uhasama, lakini sasa tumewabadilisha wamekuwa vyama vya siasa.

Lakini ile kitu bado ipo kwenye mindset (mawazo) yao, iko palepale wanafikiria kwamba CUF lengo lake ni kwamba lazima itawale Zanzibar na ikitawala Zanzibar itafanya mambo ya tofauti sana na CCM.

CCM nayo inaona haiwezi kukubali kwa sa-

babu hiyo ndiyo maana unakuta kule siasa ni ngumu kidogo.

Pambazuko: Kwa hiyo unaonyesha kwamba kuna tatizo la kihistoria Zanzibar, lakini kwa upande mwingine unasema angalau Muungano umewezesha kidogo mambo yakawa sawa, sasa tatizo la kihistoria linasuluhishwa vipi?

Sumaye: Ni kweli Muungano pamoja na hili la kuwepo Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hilo la kihistoria linahitaji tu kuelimishana kwamba watu waelewe kwamba yale mambo ya zamani sasa yameisha na tunakwenda kwenye ukurasa mpya wa maelewano, siyo wa kusema hawa walichukua nchi yetu.

Pambazuko: Unadhani kuna haja ya kuungalia Muungano, hasa muundo wake wa sasa?

Sumaye: Tunasema Muungano umelinda hata uhai wa Zanzibar.

Nakumbuka hata Mwalimu Nyerere alisema kama siyo Muungano, Waunguja na Wapemba hawatakaa pamoja na baadaye huko Zanzibar kutakuwa na Wazanzibari na Wazanzibara.

Kwa hiyo, Muugano umekuwa muhimu sana katika jambo hilo.

Sasa structure (muundo) ya Muungano kwamba utaifanya Zanzibar iwe stable (imara) zaidi, mimi nasema siku zote nimekuwa advocate (mtetezi) wa serikali mbili. Unajua watu wengi wanafikiri serikali tatu.

Mimi argument (hoja) yangu ni moja tu as long as (iwapo) tunataka Muungano uendelee, ser-



Inaendelea Uk. 28

Kichina chavutia wanafunzi wengi

Na Mwandishi WETU

LUGHA ya Kichina, inaonyesha dalili za kukua kwa kasi nchini Tanzania, kwa kuwepo idadi inayoongezeka ya watu wanaoizungumza na kuanika.

Hali hiyo inathibitishwa na takwimu za Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) zinazoonyesha ongezeko la wanafunzi wanaojifunza lugha hiyo shuleni.

Necta ikitangaza matokeo ya kidato cha sita kwa mwaka huu, 2024, wiki iliyopita, imeeleza kuwa idadi ya wanafunzi waliosoma tahasusi inayohusisha lugha ya Kichina. iliongezeka kutoka 19 mwaka 2023 hadi 43 mwaka 2024.

Msukumo wa Watanzania kupenda kujifunza lugha hiyo inayotumiwa na taifa kubwa - la pili kiuchumi duniani, China, unatokana na kuongezeka kwa uhusiano, hasa wa kibiashara, kwa nchi hizi mbili.

Katika miaka ya hivi karibuni idadi ya wafanyabiashara wa Kitanzania wanaokwenda China kununua bidhaa imekuwa ikiongezeka.

Lakini kwa upande mwingine, China nayo imeongeza mikakati yake ya kusambaza mafunzo ya kuandika na kuzungumza lugha hiyo duniani.

Katika mawanda ya kimataifa, Kichina kinatajwa kuwa lugha ya kwanza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu wanaokifahamu vyema. Kiingereza kinafuatia na baadaye Kihispania.

Katika jitihada za kukuza lugha yake Tanzania, China imekisaidia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzisha taasisi iitwayo Confucius, inayofundisha lugha ya Kichina.

Aprili mwaka huu, taasisi hiyo ilitoa msaada wa vitabu 100 vya kufundishia lugha hiyo kwa Shule ya Sekondari Mtakatifu Mathew iliyopo Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani.

“Taasisi hii imekuwa ikifundisha lugha ya Kichina, mpaka sasa wanafunzi 100 wamenufaika kwa kujifunza na wengine wamepata ufadhili wa masomo ya elimu ya juu nchini China,” alisema Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Zhang Xiaozhen.

Somo la Kichina liko katika tahasusi za lugha yaani Kiswahili, Kiingereza na Kichina (KLC), na kwamba watahiniwa waliopata daraja la kwanza kwa mwaka 2024 ni 33 sawa na asilimia 76.74 kutoka watano au asilimia 26.32 wa mwaka 2023.

Akitangaza matokeo hayo pamoja na mambo mengine, Katibu Mtendaji wa Necta, Dkt. Said Mohamed alisema ufaulu kwa ujumla mwaka huu umepanda kwa asilimia 0.26 ukilinganishwa na mwaka uliopita.

Baraza hilo limeeleza kuwa jumla ya watahiniwa 113,504 walifanya mtihani huo wa kidato cha sita mwaka 2024 katika shule 931 na vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 258.

Akizungumzia kuhusu masomo ya lugha Dkt. Mohamed alisema yana ufaulu mzuri ambao ni kati ya asilimia 96.84 hadi 100.

Hisabati bado pasua kichwa

Necta imeonyesha kwenye matokeo hayo kuwa ufaulu wa watahiniwa wa shule kimasomo unaonesha kuwa masomo yote yana watahiniwa waliofaulu kati ya asilimia 96.84 hadi 100 isipokuwa somo la Hisabati ambalo watahiniwa wamefaulu kwa asilimia 77.55.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Confucius ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inayofundisha lugha ya Kichina (CI), Profesa, Zhang Xiaozhen, akimkabidhi kitabu mwanafunzi Rahel Njovu, baada ya kutoa msaada wa vitabu kuwawezesha wanafunzi wa Shule ya Sekondari St. Mathew kujifunza Kichina. (Picha na Mtandao)



Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

Inatoka Uk. 26

ikali mbili ndiyo nafuu sana.

Utakapofanya serikali tatu, achana na suala la gharama na gharama iko kweli, lakini utakapofanya serikali tatu, tatizo litahama kutoka Zanzibar itakuwa kati ya Tanganyika na Jamhuri ya Muungano.

Kwa sababu (Tanzania) Bara leo ina watu milioni 60, Zanzibar ina watu karibu milioni moja, kwa urahisi sema tu 65 kwa milioni mbili.

Mimi ni Rais wa Tanganyika na wewe ni Rais wa Jamhuri, mimi nina watu milioni 65 wewe una watu 67 kwa hiyo kama ni pesa zinatoka kwangu kama ni power (nguvu) inatoka kwangu.

Hata majeshi ambayo utasema yako chini yako, lakini ni watu wangu. Ninaweza nikakuheshimu, lakini pia naweza nisikuheshimu.

Nisipokuheshimu vurugu itakuwa kati ya Tanganyika na Jamhuri ya Muungano na hilo litakuwa tatizo kubwa mara elfu kuliko hili la Zanzibar tunaloliona.

Pambazuko: Unazungumziaje rushwa ndani ya vyama vya siasa, unadhani bado ni tatizo?

Sumaye: Rushwa ni kubwa zaidi hivi sasa, tena kubwa sana ni terrible (mbaya). Hata wewe leo ukitaka kugombea ubunge, kitu cha kwanza watu watakachokuuliza ni una hela? Hata mke wako atakuuliza una hela?

Kwa hiyo, hali ya rushwa sasa hivi sijui hata kama wanaita tena rushwa, yaani kama imekuwa halali fulani hivi, kama huna hela kwa kweli usiende kuhangaika ni too bad (mbaya sana).

Sasa imefika mahali watu wanasema aaah kila kitu kina gharama bwana... lakini ukweli ni rushwa.

Kwa hiyo watu wengi ambao tuseme wangetamani kuingia kwenye siasa, lakini hawana fedha, maana yake wamefungiwa nje. Hii ni hatari sana.

Watu wenye fedha hata kama hawana uwezo, wanaingia kwenye siasa kwa sababu wana fedha.

Hiyo ni hatari.

Sasa sijui tufanyeje, lakini ukweli hali si nzuri na ni vyama vyote; CCM na upinzani, wote sasa hivi hali ni hiyo hiyo kama huna fedha hupiti.

Pambazuko: Sasa katika hilo unashauri nini kifanyike?

Sumaye: Hata mimi sijui cha kufanya zaidi ya kusema tuelimishane na tupige vita.

Kwa sababu imefika mahali hata wananchi wa kawaida ukiwauliza wanasema tunaangalia anayetupa nyingi zaidi ndiye tutakayemchagua wanakwambia kabisa hata mimi mwenyewe nimewauliza mara nyingi.

Huwa nikiwauliza watu kadhaa labda katika hawa watu (wanaotaka kugombea) mnaonaje, wanakwambia sisi tunangalia hela na wao si tunawapelekea huko bungeni wakapate hela kwanini sisi tusifaidi?

Na kweli kuna mahali fulani waliniambia hadi sasa hivi aliyetoa nyingi ni fulani anayefuatia ni fulani wa tatu ni fulani... kwa hiyo sisi tumesema hawa watatu tunawapanga kwa namna hii hii na kweli katika uchaguzi wanatoka hivyo hivyo.

Pambazuko: Ukiwa ni mwanasiasa na kiongozi mwandamizi wa serikali, ni dhahiri wewe ni kimbilio hasa kwa vijana kuja kuchota busara, unaona nchi inakuthamini?

Sumaye: Unajua tumejiweka katika sura ambayo leo kwa mfano mimi nikizungumza mambo haya watu watakusikiliza kweli, lakini baadaye waliopo madarakani wataanza kukuwekea labda nongwa hivi.

Huyu hajui kama muda wake umepita na hivi na vile. Kwa hiyo mara nyingine inafika mahali unasema hebu ngoja nijinyamazie tu.

Pambazuko: Kwa hiyo tunarudi palepale kwenye mifumo kuwa imeshindwa kujitengeneza ili muendeleo kuinufaisha nchi?

Sumaye: Nadhani kuna ukweli hapo, mimi sitaki ndiyo maana unaona hatusemisemi, kama mtu akitaka, tukipata nafasi ya kuonana ya kumshauri, unamshauri, lakini ukisema sema unaweza kuonekana vibaya.

Pambazuko: Rais au waziri mkuu wa sasa wanakuomba ushauri?

Sumaye: Labda itokee mara moja moja sana,

Inaendelea Uk. 29



Inatoka Uk. 28

lakini kawaida hawaombi.

Pambazuko: Kwa hiyo na wewe ukiwa na jambo limekugusa sana unataka kumshauri Rais Samia huwa unafanyeje?

Sumaye: Nafanya hivyo mara moja moja, unaweza kupata nafasi, lakini mara nyingi ni vigumu sana kumfikia kama ni rais na nadhani she is too busy (ana kazi nyingi sana) na unaona kweli hakai, leo yuko huku kesho kule inawezekana ni suala la kutingwa na majukumu.

Pambazuko: Kwa ujumla maisha ya ustaafu uwaziri mkuu yakoje kwako?

Sumaye: Aaah... ninaishi kama mwananchi wa kawaida, ingawa siyo sana, maana serikali inanipa gari, lakini nakuwa huru nafanya mambo yangu.

Naweza kwenda shambani wakati wowote nitaka japo kilimo ni kigumu.

Tangu zamani maisha yangu hayajabadilika sana, hata nilipokuwa waziri mkuu, sikuwa na mbwembwe za uwaziri mkuu, nilikuwa tu mtu wa kawaida, nafanya kazi zangu za uwaziri mkuu.

Sasa nimestaafu nafasi hiyo, nafanya kazi zangu za kawaida. Mimi na-enjoy (nafaidi) maisha, sina makuu.

Pambazuko: Mzee Mkapa kwenye kitabu chake aliandika mambo ambayo kama angeweza kurudisha nyuma angerekebisha, wewe katika miaka kumi ya uwaziri mkuu ungerudi leo, ni kitu gani ambacho ungefanya tofauti na ulivyofanya wakati ule?

Sumaye: Unajua waziri mkuu ni mtendaji wa sera ya serikali, anasimamia utendaji wote, kwa hiyo sera zikishapitishwa na rais au na chombo chochote, wewe unasimamia.

Mimi uki- niambia tu kitu cha ujumla ambacho some-times (wakati mwingine) nafikiri - sijui kama leo nafikiri hivyo-hivyo, ni kwam-b a



Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa, Muungano

wakati ule nilikuwa nafikiri Afrika na hata Tanzania, tulikuwa hatujafikia sana wakati wa kudandia demokrasia kama zilivyo kwa wenzetu.

Elimu ya demokrasia haijatingia na ndiyo maana hata kila siku mtu akiingia mpya, anaanza mambo mapya, hatujaji-tune (hatujajipanga) sawasawa kama wenzetu.

Kama nilivyosema systems (mifumo) haziko sawasawa.

Nakumbuka niliwahi kumwambia hata rais wangu wakati huo Mzee Mkapa, kwamba kama siyo hii demokrasia, hivi hii nchi chini ya direction (mwelekeo) yako ningeipeleka kwa kasi zaidi.

Lakini ukweli na ndiyo maana unakuta kwa mfano nchi kama Rwanda wanasema kuna demokrasia ya uchaguzi, ukweli ni kwamba hakuna, ni amri moja.

Lakini si unaona inavyokwenda na hata hivyo kiongozi wake anaogopaogopa kwa sababu anajua watu watasema.

Lakini ingelikuwa anakwenda tu, angeweza kwenda mbali zaidi kwa hiyo sometimes (wakati mwingine) huwa nafikiri labda mambo yetu haya ya Kiafrika ni yale yale, mnaambiwa fanyeni hivi tunafanya.

Mimi sipendi kiongozi mmoja anang'ang'ania madarakani, lakini tungeweza kuwa na mfumo ambao hauweki breaks (vizungiti) ambazo hata kama mtu una nia njema breaks zimejaa.

Unataka breaks ziwepo pale ambapo unaona huyu mtu anatupeleka vibaya.

Kwa hiyo kuna vitu vingine vya namna hiyo. Vitu vingi ambavyo tulivifanya vingi sasa hivi kama regulatory authority (mamlaka za udhibiti) nyingi sioni kama zinafanya tena kazi.

Tulianzisha kwa nia njema, hata sheria ya Benki Kuu naona haifanyi kazi kama inavyotakiwa.

Mfano, Benki Kuu kazi yake ni kusimamia

Ana kwa Ana

Maneno 3,000 ya Sumaye akizungumzia Uongozi wa Samia, rushwa....

Inatoka Uk. 28

uchumi na kutunza hela ya serikali, lakini at some points (wakati mwingine) unakumbuka fedha zilichukuliwa na hela ambayo siyo ya serikali ziliingizwa Benki Kuu.

Ukishafanya hivyo, maana yake umekomba hela mitaani, kwa hiyo watu hawawezi kuwa na hela.

Lakini kwa sheria, sisi tulizopitisha maana na tuwahi kufanya reform (mabadiliko) kwenye financial Institution (taasisi za fedha) ambazo ni pamoja na Benki Kuu.

Rais alikuwa hawezi kuagiza Benki Kuu yeye mwenyewe kama mtu tu hivi, hapana, bali kuna mfumo ambao upo.

Baadaye ikawa sasa rais anaagiza. Ikishafika hapo hata gavana atasimamia vipi uchumi?

Siku moja niliwahi kumwuliza mkuu wa Ewura (mamlaka ya udhibiti wa nishati), nikamwambia hebu nieleze wewe unaelewa Ewura ni nini? Akasema naelewa.

Nikamwambia ni regulatory authority (mamlaka ya udhibiti) inakuwaje wewe unapanga bei ya mafuta? Wewe umeshakuwa price commissioner (kamishina wa bei)?

Akakibu aaah unajua ooh tunapewa maagizo.

Nikamwambia regulatory authority haitakiwi ipewe maagizo na mtu yeyote kwa sababu regulatory authority, anaiweka kama taasisi ya katikati.

Serikali ikiweka bei fulani na consumer (mlaji) anaona hii bei si sahihi wewe regulatory authority ndiyo unasimama katikati unamwita serikali, unamuuliza akuambie alifikaje kwenye hii bei na wewe consumer kwanini unalalamika.

Sasa wewe ndiyo utawasikiliza unaamua utaiambia serikali hiyo siyo.

Kwa vile Ewura inapanga bei ya mafuta sasa mtu asiporidhika na ile bei anaenda wapi? Hivyo mifumo imevurugika sana, lakini aaah tuendelee tu.

Pambazuko: Hizi mamlaka za usimamizi zote

mlizianzisha ninyi unadhani kwa mazingira ya sasa tunahitaji zingine tena au zilizopo zinatosha?

Sumaye: Inategemeana. Kama serikali inaweza kuona kwamba kuna mahali kuna uhitaji wa regulatory authority iifanye, lakini hazitakiwi kuwa nyingi kwa sababu ni mzigo. Zinatakiwa tu ziwe na kazi za kutosha.

Swali: Kati ya CCM na Chadema pengine ni wapi ambapo ulikuwa na amani zaidi?

Sumaye: Kwenye siasa hakuna raha. Kila mahali pana changamoto.

CCM nilikuwa kiongozi na sikuwa na changamoto za mimi mwenyewe.

Chadema ina changamoto sana kwa sababu kimsingi kama nilivyosema, nilikwenda kule kutoa elimu ili kujenga kile chama kikae vizuri.

Kwa hiyo nilikuwa kidogo frustrating (kukatisha tamaa) kwa sababu unaelekeza hivi leo wanakubali, kesho tena wanarudia yale yale.

Nilipotoka tu Chadema watu wengi walini fuata kuwa nianzishe chama, nisirudi CCM. Na ni wengi sana walini fuata, lakini niliwaambia sina hela ya kufanya hivyo, wakasema hela watanitafutia ziko nyingi na wakati ule Magufuli ndo mkuu wa nchi.

Sababu nyingine nikawaambia umri wangu umeshakuwa mkubwa na siwezi kuanza tena kukimbizana na vyama, acha tu nibaki kuwa mshauri wa chama chochote.

Hadi leo niko tayari chama chochote kikihitaji ushauri nitafanya kwa moyo mmoja.

Pambazuko: Miongoni mwa watoto wako kuna ambao wamefuata nyayo zako kwenye ulingo wa siasa?

Sumaye: Unawajua kila mtu ni mwanasiasa. Mfano labda serikali ikifanya jambo fulani ambalo hulipendi, si utasema aaah hii nini tena.

Hivyo watoto wangu wako jumla wa kiasi hicho, lakini akijitokeza mmojawapo nitashukuru. Pambazuko: Hujawahi kumshawishi mmojawapo labda agombee nafasi yoyote ya kisiasa?

Sumaye: Sijafanya hivyo. Kilichowakatisha tamaa zaidi watoto wangu ni rushwa. Wanataka siasa kama za enzi zangu, lakini sasa hivi hazipo.

Mimi sikuwahi kufanya siasa za rushwa kwa miaka yote 20 ya kugombea ubunge. Sijawahi kuhonga hata ukienda wilayani watakwambia.



Mtuhumiwa uhalifu wa kivita Uswisi aponda raha mafichoni Afrika Kusini



Christoph Huber

Na Ra'eesa Pather, Luvano Ntuli, Jane Borman

MAISHA yake yamegubikwa na usiri mkubwa mno. Hataki kujulikana wala hana uhusiano na watu wengi, isipokuwa wachache sana anaofanya nao biashara.

Hayupo kwenye mitandao ya kijamii kwa jina lake na hapendi kupigwa picha. Hana picha nyingi kwenye mitandao, isipokuwa mbili tu ambazo haijulikani nani alimpiga na zilipigwa akiwa wapi.

Pamoja na kuishi maisha hayo, Christoph Huber ni miongoni mwa matajiri wakubwa “wanaoogelea” juu ya fedha nyingi mno.

Utajiri wake unadaiwa kupatikana kwenye

biashara ya silaha, hasa kwa kuuza kwa makundi yanayotajwa kuhusika kwenye uasi na ugaidi.

Kwamba Chris, kama ilivyogundulika kupenda kuitwa, anahusika pia kuuza silaha kwa makundi yanayopigana vita dhidi ya serikali, mengi yakiwa kwenye ardhi ya Afrika.

Kutokana na biashara yake hiyo, inayohisiwa anaifanya kwa kushirikiana na matajiri wengine kutoka nchi tajiri - kunakotengenezwa silaha, Chris, anasakwa kwa udi na uvumba ili kujibu mashitaka ya uhalifu wa kivita yanayomkabili nchini Uswisi.

Chris, amekuwa akijificha, anakoishi kume-kuwa kukielezwa kwamba hakujulikani, lakini wiki kadhaa zilizopita, uchunguzi wa Taasisi ya Open Secrets, “umemuibua.”

Taasisi ya Open Secrets, imebaini kuwa Chris, anaishi kwa kujificha ndani ya eneo lililojitenga zaidi – wanakoishi matajiri, Somerset West, nje kidogo ya Jiji la Cape Town, nchini Afrika Kusini.

Uchunguzi wa taasisi hiyo, ambao umechapishwa kwa mara ya kwanza na gazeti la The Continent – linalofanya kazi na Pambazuko, umebaini kuwa nyumba anayoishi Chris, aliinunua Mei, 2018, kwa kiasi cha shilingi bilioni tatu, na baadaye kuifanyia ukarabati mkubwa, hivyo thamani yake inaweza kuwa maradufu.

Taarifa zilizopatikana baada ya uchunguzi huo wa Open Secrets, zinadai kuwa utajiri wa Chris, “umefumwa kwa damu za watu” wanaokadiria kufikia milioni sita, waliouawa kwenye “vita” vinavyoendelea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mbali na vifo hivyo vilivyotokana na vita DRC, pia kuna mamilioni ya watu wanaoendelea kuuawa ndani ya Angola, Timor Mashariki, Myanmar na maeneo mengine.

Zipo taarifa zingine zinadai kuwa Chris, ni dalali tu, ambaye anafanya biashara hiyo ya kuuza silaha, kwa niaba ya matajiri wenzake.



Uhalifu

Mtuhumiwa uhalifu wa kivita Uswisi aponda raha mafichoni Afrika Kusini

Inatoka Uk. 31

Inaelezwa kuwa Chris, raia wa Uswisi, alianza biashara hiyo miaka ya mwanzo ya 1990 na kwamba anaendelea nayo hadi sasa.

Akana kutajirika kwa damu

Chris amekuwa akikanusha mara kwa mara, kutoka mafichoni, kwamba anahusika na utajiri wenye “kujaa damu” za watu – wengi, wasiokuwa na hatia.

Kwamba hatua ya kuwa mfanyabishara wa silaha kwa waasi na magaidi, anaruhusu kupokea fedha zinazotokana na bidhaa anayouza kutumika kuua.

Kupitia kampuni ya mawakili, Chris amekuwa akisema kuwa “yeye ni mfanyabiashara halali na anafanya hivyo kwa bidhaa halali kwa wanazohitaji.”

Anasakwa na Uswisi

Imefahamika kuwa tayari Chris ana uraia wa Afrika Kusini na kwamba anamiliki nyumba nne za kifahari katika maeneo wanayoishi matajiri wakubwa.

Kufahamika huko kunamaliza minong’ono ya wapi alipo Chris, na sasa ni kazi kwa taasisi za haki, ikiwamo mahakama, kufanya kazi kumkamata na kumfikisha mbele ya sheria.

Chris, anasakwa na nchi yake Uswisi, ambako anatakiwa kwa ajili ya kujibu mashitaka ya uhalifu wa kivita dhidi ya binadamu.

Mawakili watishia

Mawakili wa Chris baada ya kugundua kuwa mteja wao anachunguzwa na kwamba Open Secrets imebaini alipo, walitishia kuchukua hatua za kisheria dhidi ya taasisi hiyo na endapo wangechapisha matokeo ya uchunguzi wao waliowataka usitishwe.

Ukaribu na Rwanda

Open Secrets imebaini kuwa kuna uhusiano wa karibu zaidi wa shughuli za Chris, na kampuni kadhaa nchini Rwanda.

Hiyo inatokana na kuonekana kwa baadhi ya mawasiliano ya siri ambayo yanadhihirisha

kuwepo kwa “biashara yenye shaka – ya kuuza silaha.”

Nyaraka zilizoonwa zinaweka wazi kwamba Februari 2001, Chris alisaini mkataba kwa nia-ba ya kampuni ya Rwanda ya Medivals Minerals and Sominki na Société Minière et Industrielle du Kivu - kampuni inayomilikiwa na DRC kwa ajili ya kufanya biashara.

Kampuni hiyo ya DRC ilimiliki zaidi ya kilomita 100,000 za uchimbaji madini ya coltan, cassiterite na wolframite huko Kivu Kaskazini na Kusini Mashariki ambayo ilikuwa inamilikiwa na RCD-Goma mwaka 1998.

Chris adaiwa kupora madini

Mbali na madai ya kuhusika kuuza silaha, Chris pia aliorodheshwa katika ripoti muhimu ya mwaka 2009 kuhusu uporaji wa madini mashariki mwa DRC, iliyotolewa na Kundi la Wataalamu wa Umoja wa Mataifa kuhusu DRC.

Ilisema kuwa kampuni ya African Ventures, ambayo ilimwajiri Chris akiwa mshauri, ilinunua madini kutoka kwa kampuni ya China, Huaying Trading Company (HTC), ambayo ilinunua cassiterite kutoka maeneo yaliyodhibitiwa na wanaotajwa kuwa waasi wa Rwanda.

Shutuma zaidi za hivi karibuni dhidi ya Chris zimo katika ripoti ya uchunguzi iliyotolewa na serikali ya sasa ya DRC iliyochapishwa Aprili, mwaka huu.

Pia ipo ripoti nyingine ya mawakili wa Marekani; Amsterdam and Partners, inayoeleza kuhusu madai ya kutoroshwa madini kutoka DRC na kumtaja Chris mara 33, ikimwita yeye na washirika wake wa kibiashara kuwa ni “msingi wa mitandao ya magendo ya Rwanda katika Afrika ya kati.”

Makala haya ya uchunguzi, yamechapishwa kwa mara ya kwanza na The Continent, gaze-ti linalosambazwa kwa njia ya WhatsApp na kuchachapishwa kwa lugha ya Kiingereza. Unaweza kupata nakala yake bure, kila wiki kwa kujiandikisha kupitia namba hii: +27738056068



Risasi yaongeza umaarufu kwa Trump



Donald Trump akiwa na maofisa usalama baada ya risasi kuparaza sikio lake katika mkutano wa hadhara huko Pennsylvania katika jaribio la kumuua. (Picha kutoka Getty Images)

Na Mwandishi WETU

MITANDAO ya kijamii imehemewa na salamu za pole na kumtakia kupona haraka Donald Trump, rais wa zamani wa Marekani ambaye alijeruhiwa kwa risasi.

Juzi, Jumamosi, Trump akiwa kwenye mkutano wa kampeni za kuwania kurejea Ikulu ya White House, Washington, D.C, aliparazwa na risasi ya mtu ambaye alikuwa na lengo la kumuua.

Taarifa zilizofika kwa gazeti la Pambazuko zinazeleza kuwa akiwa kwenye kampeni katika eneo la Butler, Pennsylvania, aliparazwa kwa risasi katika sikio lake la kulia, na kumsabaishia maumivu.

Baada ya risasi kusikika kutoka kwa waliohudhuria mkutano wake, maofisa usalama walimzinga, lakini tayari alikuwa amejeruhiwa.

Aliyejaribu kumuua mgombea huyo wa urais kwa tiketi ya chama cha Republican, aliuawa kabla hajaleta madhara zaidi.

Kutokana na shambulio hilo, takwimu zinaonyesha kuwa umaarufu na hata kuungwa mkono kwa Trump kwenye kuwania urais wa nchi hiyo, kumeongezeka maradufu.

Uchaguzi wa Marekani umepangwa kufanyika Novemba 5, mwaka huu, huku wagombea wawili

wakiwa wanachuana vikali. Wagombea hao ni Joe Biden, rais wa sasa – kupitia chama cha Democratic na Trump.

Nguvu za wagombea wawili

Tangu kuanza kwa kampeni za uchaguzi huo, Rais Biden alikuwa akipewa nafasi kubwa ya kuitabaka mshindi, hata hivyo, hali ilibadilika wiki mbili zilizopita baada ya kufanyika kwa mdahalo kwa wagombea hao.

Mdahalo huo “ulipindua meza” baada ya Rais Biden, kuonyesha udhaifu wa kujibu hoja za mpinzani wake, Trump na kibaya zaidi, kiongozi huyo wa Marekani akithibitika kuwa na changamoto ya “kusahausahau vitu.”

Rais Biden (81) alionekana kukwama kuwavutia hata wafuasi na wapenzi wake, kwani alishindwa kung’ara, hivyo matarajio yao ya kupata ushindi wa mapema kwenye uchaguzi yakaanza kufifia.

Kutokana na hali hiyo, wasaidizi wake na marafiki wakamshauri Rais Biden kujiondoa mapema kwenye kinyang’anyiro kwa madai kuwa atashindwa na Trump.

Pamoja na ushauri huo, wahafidhina ndani ya chama chake na watu wengine, hasa “wazee wenzake”- wamekataa kujiondoa, na kumtaka aendelee kufanya kampeni kwa nguvu zaidi.

Wakati haya yakitokea, upande wa Trump, nyota yake imeendelea kuonekana iking’ara zaidi na kwamba sasa anapewa nafasi ya kuwa rais mpya wa taifa hilo kubwa kiuchumi na kivita duniani.

Wagombea walionusurika kifo

Kusikika kwa milio ya risasi na hata wagombea urais wa Marekani kushambuliwa, siyo mara ya kwanza kwenye historia ya nchi hiyo.

Wapo walioshambuliwa na hata wengine kuuawa, miongoni mwao ni pamoja na George Wallace ambaye mwaka 1972, akiwa katika kampeni za kuteuliwa kuwa mgombea wa kiti cha urais wa Democrats alipigwa risasi nne na kupooza maisha yake yote.

Robert F. Kennedy mwaka 1968, ambaye alikuwa anawania uteuzi wa urais kwa chama cha Democratic, alipigwa risasi na kuuawa katika Hoteli ya Ambassador, Los Angeles, California.

Ziara ya Rais Samia Katavi

Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika matukio tofauti wakati wa ziara yake mkoani Katavi jana. (Picha zote na Ikulu)





*Mchekesha-
ji Eric
Omondi
(mwenye
nywele
nyekundu),
akiwa
kwenye
maanda-
mano ya
kupinga
mfumuko
wa bei nchi-
ni Kenya
(Picha na
Mtandao)*

Ruto akiona cha moto kwa Gen Z

Na Julius MKAMBI

RAIS William Ruto wa Kenya wakati wa kampe-
ni kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2022, ali-
penda kutumia neno la 'Hatupangwigwi.'

Usemi huo uliogeuka kuwa maarufu sana uli-
tokana na wimbo maarufu wa vijana wa muziki
wa kizazi kipya, ikiwa na maana kwamba "vijana
hawataruhusu kupangiwa kwenye jambo lolote."

Alitumia neno hilo kama ishara ya kuto-
kukubali shinikizo la mtagulizi wake, Rais Uhu-
ru Kenyatta aliyemuunga mkono mpinzani wake
kisiasa, Raila Odinga, huku akimtaka Ruto ku-
subiri kidogo kutimiza azma yake ya kuwa Rais
wa Kenya, kwa maana ya kumuachia uongozi
mpinzani wake.

Aidha, ni neno ambalo Rais Ruto alilitumia
mara nyingi kuhamasisha vijana kutoruhusu
mtu kuwapangia jambo lolote ambalo wamed-
hamiria kulitekeleza.

Takribani miaka miwili tangu kuchukua
hatamu ya uongozi, vijana maarufu Gen Z wa-
nalitumia neno hilo hilo 'Hatupangwigwi' kwa

kufanya maandamano ya amani nchini nzima
kupinga utawala wa Rais Ruto.

Ni maandamano ambayo chimbuko la
uhamasishaji wake ulikuwa mitandao ya kijamii
na hayakubagua kabila, dini, jinsi au maeneo
fulani ya nchi kama ambavyo yamekuwa yaki-
shuhudiwa kwenye maandamano ya miaka ya
nyuma.

Vijana wa Gen Z walianza kushinikiza
wabunge kuukataa Muswada wa Fedha 2024 na
licha ya wabunge kuupitisha, Rais Ruto alikataa
kuweka saini na kuurudisha bungeni, chombo
ambacho kina mamlaka ya kuutupilia mbali.

Rais Ruto baadaye alisema atabuni kamati
itakalojumuisha sekta mbalimbali ikiwemo pia
vijana wa Gen Z, kwa lengo la kujadili mus-
takhabali wa taifa.

Hata hivyo, Gen Z ambao hawana viongozi
maalumu wanaofahamika, hawataki majadilia-
no na serikali kwa kile wanachosema majadilia-
no yamekuwa mengi tangu tawala zilizopita na
wanahisi hakuna jipya litakalotoka kwenye ma-



Kenya

Rais Ruto akiona cha moto kwa Gen Z



Wananchi wakiwa kwenye maandamano ya kupinga Muswada wa Fedha nchini Kenya. (Picha na Mtandao)

Inatoka Uk. 31

jadiliano anayoitisha Rais Ruto.

Hata hivyo, wanachokitaka vijana wa Gen Z kutokana na orodha ya masharti yao waliyochapisha mitandaoni ni kutaka kuona na kuthibitisha kuwa serikali anayoongoza Rais Ruto inawajibika zaidi kwa Wakenya.

Wanataka serikali kuheshimu uamuzi wa mahakama na kufutilia mbali vyeo visivyo halali kikatiba, ikiwamo naibu mawaziri, pamoja na kuondolewa ufadhili wa pesa za umma kwa ofisi za mke wa rais, mke wa naibu rais na mke wa mkuu wa mawaziri na badala yake fedha hizo zielekezwe kuajiri walimu na madaktari.

Orodha hiyo ya masharti ya Gen Z kwa Rais Ruto pia inataka kufutwa kwa kodi ya majengo, kuchapishwa kwa rekodi zilizokaguliwa za matumizi yote ya fedha za umma.

Rais Ruto katika kuhakikisha anatuliza joto la Gen Z, lililopanda ni kuamua kuwaondoa kazini maofisa wa serikali walio na rekodi ya uhalifu na masuala ya kukosa uadilifu.

Pia joto la Gen Z linataka kuwepo kwa uongozi thabiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mi-paka (IEBC) na kutangazwa kwa uongozi wa tume hiyo.

Waandamanaji pia wanataka walimu, maaskari, madaktari na wauguzi kuongezwa ishahara kama ilivyofanyika kwa mawaziri, wabunge na majaji.

Katika orodha ya mambo wanayotaka vijana hao wa Gen Z, ni Tume ya Kurekebisha Mishahara kutangaza haraka nyongeza ya mishahara kwa watoa huduma, badala ya kuwapa ujira na marupurupu manono kwa “wakubwa.”

Waandamanaji hao wanasisitiza kuwa wabunge hawafai kupata zaidi ya madaktari, na kupendekeza mishahara na marupurupu yao kupunguzwa ili wapokee shilingi 200,000 za Kenya (sawa na Sh4 milioni) kwa mwezi.

Kukataliwa kwa Muswada wa Fedha kuna-tokana na ongezeko la kodi kwenye bidhaa muhimu, ikiwamo chakula, mafuta na bidhaa zingine muhimu kwa makisha ya kila siku.

Kilio kingine cha waandamanaji hao ni madaidai kwamba hawaoni namna nzuri kodi zao wanazokatwa zikitumika ipasavyo, hivyo Gen Z wanamtaka Rais Ruto kupunguza “anasa na matumizi yasiyo na maana.”

Tayari Ruto ametangaza kupunguza baadhi ya matumizi makubwa ya serikali anayoongoza.

Sharti linguine ambalo linaonekana litakuwa ngumu kwa Ruto, ni kujiuzulu na hata alipoulizwa swali hilo kutokana na Wakenya kushindwa kuwa na imani naye, alisema ana wajibu kutimiza kiapo alichokula nalo ni kulinda Katiba, hivyo haoni sababu za kuondoka madarakani kwa shinikizo wakati “kuna meza ya mazungumzo.”

Mwanaharakati na mkongwe wa sanaa ya uchekekeshaji, Eric Omondi, amesema kuwa “bado maanamao hyataendelea” hadi pale Rais Ruto atakapoacha kuwaona wananchi wa Kenya ni wajinga na kwamba hawaelewi lolote kuhusu katiba na haki zao.

Omondi, ambaye amejitokeza kuwa mkongoni mwa vinara wa maandamano hayo, amesema kwamba wakati wa kutaka manbadiliko makubwa kuendesha serikali.

“Tunataka serikali inayowatumikia Wakenya wote kwa usawa na haki, na siyo ile inayobeba wanasiasa na kuwasujudu matajiri, huku ufukara ukiongezeka, hii hatuwezi kukubali kamwe,” amesema mwanaharakati huyo ambaye amekuwa akisulubiwa mara kwa mara na vyombo vya dola, kila yanapotokea maandamano.

Afcon



Iwe ni Pamoja ‘Mamantilie’ Afcon 2027

Na John MARWA

WAKATI Afrika Mashariki ikisubiri kwa hamu kushuhudia uenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2027, jitihada za kutimiza ndoto hiyo zinaonekana katika ujenzi wa miundombinu ya viwanja kwa nchi wenyeji; Kenya, Uganda na Tanzania.

Ni wazi jitihada za sasa zinaendana na muda, kwani miaka miwili kutoka leo, siyo mrefu sana, endapo waandaaji watabweteka.

Tayari viongozi wakuu wa mataifa hayo wameonyesha dhamira ya dhati kuwekeza utashi, akili na mali kuhakikisha Afrika inakuja pwani ya Afrika Mashariki katika Bahari ya Hindi.

Ni nyakati ambazo tunapaswa kuhakikisha Afrika Mashariki inauza kila chema; kuanzia vivutio vya asili, utalii, utamaduni, ukarimu na hata vyakula vipatikanavyo pwani ya Bahari ya Hindi.

Niwakumbushe tu kuwa maneno ya Kiswahili ndio ngao na kigao chetu; ‘kipofu hasahau fimbo yake -’ ni wazi katika majiji na miji, ndani ya mipaka ya Afrika Mashariki imepambwa na wajasiriamali wadogo wa kuuza vyakula.

Hawa ni maarufu zaidi kwa majina ya “Mamantilie” na “Babantilie” ambao, bila shaka, nao watakuwepo “kupamba” mashindano hayo makubwa Afrika.

Swali kubwa ni hili - je, ni mpango upi sahihi wa kuwanda kushiriki kutoa huduma kwa washiriki, wakiwamo mashabiki kutoka nje ya Afrika Mashariki?

Mara nyingi yanatazamwa maeneo makubwa ya hotel za nyota tano na migahawa mikubwa, lakini tunapaswa kutambua kuwa Afcon ni utalii.

Ni utalii ambao unaweza kumleta mjomba wake Mohamed Salah, ambaye anaweza asitamani kula kwenye hoteli ya nyota tano akahitaji kula sambusa inayochomwa na Mamantilie. Je, mazingira yameandaliwa?

Lazima Mamantilie na Babantilie waandaliwe kisaikolojia jinsi gani ya kunufaika na uwepo wa wageni wengi.

Hapa nazungumzia lugha ya kukaribisha wageni, usafi wa mazingira na uadhifu wa watoa huduma.

Je, uchumi wa Mamantilie na Babantilie unaridhisha kuhudumia Afcon katika mitaa ya Roysambu, Kibera, Mbotela (Nairobi Kenya), Keko, Buguruni, Temek Stereo (Dar es Salaam, Tanzania) na Bulambuli, Kyanjenjo, Kaliro (Kampala Uganda)?

Acha niwakumbushe hii Afcon ni ya “Waswahili” na shughuli hii ni yao, hivyo ni ngumu kuwaacha nyuma na kuwasahau kwenye jambo lao.

Kuanza kujiandaa mapema kwa watoa huduma hawa wadogo, ndiyo ujanja, na siyo kuwekeza nguvu zote kwa “matajiri” pekee.

Pamoja Afcon inapaswa kuwa jumuiishi; kwa kutowasahau wale wenye mitaji midogo, kwani nao wanapaswa kukua, na huenda michuano hii ikawa mkombozi.

Kwa kuwaandaa vyema Mamantilie na Babantilie, nchi tatu kubwa za Afrika Mashariki zitakuwa zimetimiza wajibu kwa kuwaenzi mababa wa mataifa yetu; Apollo Obote (Uganda), Jomo Kenyatta (Kenya) na Julius Nyerere (Tanzania) kwenye Pamoja Afcon 2027.



Drake ateketeza mil. 800/- kwenye bet halafu wala hajali!

New York, Marekani

MSANII wa Rap, Drake ameen-delea na tabia yake ya kucheza kamari, 'betting' ambapo hivi karibuni alibetia timu yake ya taifa ya Canada iliyokuwa inacheza na Argentina.

Drake aliteketeza kiasi cha dola za Marekani laki 3 (Sh. milioni 800) za Tanzania na kupoteza fedha hizo.

Mechi hiyo iliisha kwa Argentina kuibuka na ushindi dhidi ya Canada kwa mabao 2-0 na kusebabisha timu hiyo kutinga hatua ya nusu fainali.

Drake amekuwa na kawaida ya kubashiri katika michezo tofauti tofauti kama mpira wa miguu, kikapu na masumbwi.



Rema

alipwa bil. 8/- kutumbuiza kwenye
harusi ya mtoto wa bilionea

Mumbai, India

MWANAMUZIKI wa Nigeria Divine Ikubor maarufu kama 'Rema' amelipwa kiasi cha dola za Marekani milioni 3 (sawa Sh. bilioni 8), kutumbuiza wimbo mmoja tu wa 'Calm Down' kwenye harusi ya mtoto wa bilionea wa India, Anant Ambani.

Harusi hiyo ya kifahari imehudhuliwa na mastaa wakubwa duniani wakiwemo Justin Bieber, Adele, Kim Kardashian, John Cena pamoja na mawaziri

wakuu wa zamani wa Uingereza, Boris Johnson na Tony Blair.

Ndoa hiyo ambayo imefungwa hivi karibuni nchini India baada ya mfululizo wa matukio ya kabla ya ndoa kufanyika tangu Machi mwaka huu yaliyohudhuliwa na waimbaji kama Rihanna na Katy Perry.





Kila mchezaji Hispania kupata bil. 1/-

Na Mwandishi WETU

WACHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Hispania, jana walitawazwa kuwa mabigwa wa Kombe la Mataifa Ulaya (Euro) mwaka 2024, baada ya kuifunga England kwa jumla ya mabao 2-1.

Taarifa ambazo zimelifikia Pambazuko usiku wa kuamkia leo zinaeleza kuwa kufuatia ushindi huo, benchi la ufundi pamoja na wachezaji wote wa Hispania, watapata shilingi bilioni 1 ambazo zitatolewa na Chama cha Soka cha Hispania (RFEF).

Katika kikao cha viongozi wa RFEF kuzungumzia zawadi kwa wachezaji, wakubwa hao walisema wanaamini kila mchezaji atafurahi, huku wawakilishi wa wachezaji wakisema kuwa “hawataangusha wapenzi wao na lazima watashinda.”

Katika mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Olympiastadion jijini Berlin, Ujerumani, Timu ya Hispania ilikuwa ya kwanza kuzifumua nyavu za England katika dakika 47, baada ya Nico Williams kupiga shuti kali lililomshinda mlinda mlango wa England na kuandika bao la kwanza.

England walifurukuta na kupata bao la kusawazisha katika dakika ya 73, baada ya Cole Palmer kuzifumua nyavu za wapinzani wao.

Bao la England liliamsha moto kwa timu zote mbili zikipambana “kufa na kupona”, huku mashuti mengi yakienda kwao, kwani Hispania walikuwa wakishambulia kama nyuki.

Hata hivyo, bahati haikuwa kwa England, kwani walijikuta wakipokea bao la pili lililowe kwa kimiani na Mikel Oyarzabal dakika nne tu kabla ya dakika 90 kukamilika.

Bao hilo lilizamisha matumaini yote ya England kutawazwa kuwa mabingwa na sasa wanabaki kuwa na historia ya kuwa “namba mbili” kwenye michuano ya Euro 2024.

Endapo England ingechukua kombe hilo, wachezaji wa timu yake walikuwa wameahidiwa zaidi ya shilingi milioni 120 kwa kila mmoja ikiwa ni bonasi.

Hispania wametinga fainali baada ya kuwaondoa Uholanzi kwenye mchezo wa nusu fainali kwa mabao 2-1, huku Hispania wakitinga fainali kwa kuwatoa Ufaransa kwa ushindi wa 2-1.



Wachezaji Simba hawajaelezwa masharti muhimu

Na Mwandishi WETU

Ule mpambano wa nje ya uwanja baina ya vilabu vinavyoshiriki ligi kuu nchini unaelekea ukingo ni baada ya vilabu hivyo kukamilisha usajili wa wachezaji.

Hivi sasa maandalizi yameanza kabla mpambano wao haujahamia rasmi viwanjani.

Timu nyingi zipo kwenye maandalizi kwa ajili ya ligi hiyo inayotarajiwa kuanza mwezi ujao.

Timu za Simba na Azam zimeamua kuweka kambi zao nje ya nchi – Simba wakiwa Misri na Azam wakielekea Morocco. Yanga, ambayo imeanza maandalizi yake hapa nchini inatarajiwa kusafiri kwenda Afrika Kusini kushiriki kwenye mashindano maalum yaliyoandaliwa na Kaizer Chiefs.

Kwa jinsi usajili ulivyoenda, Simba ndiyo inaonekana ina kazi kubwa ya kuandaa timu yake kwa sababu kwa kiasi kikubwa kikosi chake kinajenwaga na wachezaji wengi wapya na pia benchi jipya la ufundi.

Kwa maana hiyo kimichezo itachukua muda mrefu sana kwa kocha kupata muunganiko na

kemia ya wachezaji wake wapya. Hivyo, kocha na wachezaji wake wanahitaji muda kutengeneza timu ya ushindani.

Kabla wachezaji wa Simba hawajaondoka Dar es Salam kuelekea Misri kuweka kambi yao, viongozi wa timu hiyo, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi na ambaye pia ni mwekezaji, Mohammed Dewji, walipata fursa ya kuwafunda wachezaji hao na walimu wao.

Katika kikao kilichofanyika Dar es Salaam viongozi waliwafpa wachezaji na walimu wao masharti makubwa ambayo wanapaswa kuyazingatia kama wachezani wa Simba.

Kulikuwa na masharti kuhusu mwenendo wao, nidhamu ndani na nje ya klabu ikiwamo kujihusisha na mahasimu wao wakubwa, Yanga.

Lakini, kwa anayezijua timu hizi kubwa za Kariakoo, hayo si masharti makubwa ambayo wachezaji hao wapya wa Simba walipaswa kuelezwa.

Kuna masharti makubwa mawili ambayo wachezaji hao hawakuelezwa.

Sharti kubwa la kwanza ambalo wachezaji hao walipaswa kuambiwa ni kuwa katika maisha yao hapo Simba basi ni marufuku kufungwa na Yanga.

Walipaswa kuambiwa kuwa kufungwa na Yanga ni jambo ambalo linaweza kukatisha mapenzi ya mashabiki kwa mchezaji, kocha au hata kiongozi.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

